

BWANA, SISI TUNATAKA

KUMWONA YESU



Asante sana, Ndugu Borders.

² Mwaweza kuketi. [Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Ukipenda.) Hakika ninayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu ya kuwa hapa jioni ya leo kuanzisha uamsho huu hapa katika jiji hili la kupendeza. Nadhani kidogo niko karibu sana na hiyo. Mnaweza kusikia vizuri huko nje? Je, mnaweza kusikia huko nyuma vizuri? Hilo ni sawa.

³ Tumekuwa tukitazamia kuja hapa kwa muda fulani. Ninaweza kukumbuka siku zangu za mwanzoni mwa huduma yangu, jinsi nilivyohudumu hapa Oregon, naye Bwana akabariki kwa njia ya ajabu sana. Hapana shaka ila kuna watu hapa usiku wa leo waliokuwa kwenye kampeni hizo huko nyuma katika mwaka wa 1948, '49, hapo, huko Portland, na Ashland, na Salem, naamini, na, loo, sijui, miji kadhaa mbalimbali, Eugene, Grants Pass. Tulikuwa na mikutano mikubwa, Bwana alibariki sana.

⁴ Na sikuzote nilitaka kurudi huku nje na kushika baadhi ya hawa samaki wakubwa wa mtoni ambao ninyi watu mnawakosa, lakini sijapata nafasi bado. Na inaonekana kana kwamba kila ninapokuja niko kwenye misheni ya kuhubiri. Lakini labda naweza, la, siwezi kustaafu, wahudumu hawastaafu, sivyo, ndugu? Kamwe hawawezi kustaafu. Kwa hiyo labda siku moja, nitaondoka tu niende pamoja na baadhi ya ndugu zangu hapa, kuvua samaki. Niliona leo, tukishuka, kila mahali tulipoangalia kulikuwa na leseni ya kuvua samaki, leseni ya kuwinda, na hiyo bila shaka ilionekana nzuri kwa mhubiri mchovu, aliyedhoofika.

⁵ Na kwa hiyo, tuna furaha sana kuwa hapa kuanzisha kampeni hii ya siku kumi hapa katika jiji lenu la kupendeza. Nasi tunatumaini ya kwamba itakuwa ni baraka kubwa kwenu na kwangu. Tupo hapa bila kusudi ila kuleta huduma yetu kwenu kusaidia kuendeleza huduma ambayo sasa mnaipigania, hiyo ni imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja. Hatuko hapa kuleta chochote tofauti, bali kuwasaidia tu ndugu zetu, kuingiza huduma yetu pamoja na yao, ku—kusonga mbele kuelekea Ufalme wa Mungu.

⁶ Kwa kweli tunaamini ya kwamba Bwana Yesu atakuja siku moja katika mwili wa kawaida, kama tu alivyotwaliwa juu, na inaonekana kwangu kana kwamba wakati huo bila shaka unakaribia. Tunapoona ishara za kila namna za Kuja Kwa—Kwa—Kwake, na Maandiko yakitimia, nasi tunashangaa

tu itachukua muda gani zaidi mpaka tutakapomwona Yule mbarikiwa ambaye tumemtazamia kwa muda mrefu sana.

⁷ Kama sijakosea, mara ya mwisho nilipokuwa Oregon, ama wakati mmoja, nilikuwa pamoja na Daktari F. F. Bosworth, mtu mashuhuri, shujaa. Alikufa akiwa na umri wa miaka themanini na minne hivi majuzi, hakufa kamwe, alilala tu. Nilienda kumwona, nami nikasikia alikuwa yuafa, ndipo nikaenda kumwona, basi nilipofika kule, maskini nabii mzee amelala kitandani mwake, nasi tukaingia mlangoni, akainua maskini mikono hiyo myembamba sana, tulikuwa ndio kwanza tumetoka Afrika pamoja kwenye kampeni kubwa, nikamshika mikononi mwangu, nikalia, “Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli, na wapanda farasi wake!” Maskini askari hodari sana wa Kristo.

Nami nikamwambia nilipokuwa kule, nikasema, “Ndugu Bosworth, ni lini ulikuwa na furaha sana katika maisha yako yote ya Kikristo?”

Akasema, “Sasa hivi, Ndugu Branham.”

Nami nikasema, “Je, unatambua ya kwamba unaenda?”

Akasema, “Hakika.”

Nami nikasema, “Kwa nini useme hivyo huku ukijua ya kwamba mauti iko juu yako sasa hivi?”

⁸ Akasema, “Ndugu Branham, yote ambayo nimetetea na kuishia kwa zaidi ya miaka hamsini, ninamtarajia Yeye kuingia kwenye mlango huo dakika yoyote anichukue pamoja Naye.”

Niliikumbuka ile *Zaburi Ya Maisha*:

Maisha ya watu mashuhuri yote
yanatukumbusha
Tunaweza kuyafanya maisha yetu adhimu,
Kwa kuachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu.

⁹ Kama... Hiyo ilikuwa ni alama ya mguu kwangu mimi, kujua ya kwamba baada ya zaidi ya miaka hamsini na mitano ya huduma kazini, akihubiri miaka mingi kabla sijazaliwa, kwamba mwishoni mwa safari, bado Yesu alimaanisha mengi zaidi kwake kuliko wakati wowote maishani mwake.

¹⁰ Na yapata saa moja kabla hajaenda kuwa pamoja na Bwana Yesu, kabla Yeye hajaingia na kumchukua, alikuwa, alikuwa amelala kitandani, amelala usingizi, kisha akaamka, akaangalia humo chumbani, mke wake akaingia, na mwanawe, wengi wa wapendwa. Ndipo akaangalia pande zote chumbani, akasimama na kupeana mikono kwa zaidi ya saa moja na marafiki zake waliokuwa wameondoka kwa miaka thelathini au arobaini, wakapeana mikono, kasema, “Vema, ninakukumbuka, ulimjia Kristo katika mkutano wangu huko Joliet. Ninakukumbuka, ulikuwa huko Montreal, wakati uliponinii... ” Na akawaita kwa jina, mtu aliyekuwa amekufa kwa miaka mingi na ameaga dunia.

Watakatifu hawafi, wanaenda tu kuwa pamoja na Bwana, hivyo tu.

¹¹ Ndipo hatimaye, baada ya kukutana na mama na baba yake, na wote, akarudi na kulala kwenye kitanda kidogo pale, akakunja mikono yake, akafumba macho yake, akaenda kukutana na Bwana. Mtu hodari namna hiyo. Nina hakika kwamba, tungeweza kuwa na majaliwa ya kuzuru Nchi hiyo kuu kabla ya Kuja kwa Bwana, kwamba tutamwona Ndugu Bosworth kule pamoja na marafiki zake, wenye furaha, wakiufurahia Uzima wa Milele kwa upeo wake.

¹² Sasa, tumekuja kwenye mji huu, kwa mwaliko wa ndugu zetu wa thamani hapa, madhehebu mbalimbali na awamu mbalimbali za imani ya Kikristo. Nasi tumekuja kuunganisha nguvu pamoja nao kwa manufaa ya jamii hii, kwa ajili ya mji huu, na kwa maeneo ya karibu, kwamba itapafanya ma—mahali pagumu zaidi pa kufanyia mabaya, baada ya mkutano huu, mahali rahisi zaidi pa kutenda haki, baada ya mkutano huu, tumekuja kuyafanya maisha kuwa matamu zaidi kwenu, kuhakikisha kwamba, kama tunaweza kuomba maombi ya imani, kwamba Mungu atawaponya wagonjwa katika jamii hii pamoja na ndugu zetu, kutoa wito kwa wenye dhambi, labda wito wa mwisho watakaopata kupokea, kwamba wataingia katika ile Nchi iliyobarikiwa ambamo waliokombolewa tu ndio wanaoweza kwenda, na hilo ndilo lililotuleta hapa, makusudi.

¹³ Kusudi letu kuu ni kuhakikisha mko tayari kwa ajili ya hilo; kinachofuata ni kuwaombea wagonjwa na kuona ya kwamba wanapona, kumwomba Bwana; na halafu jambo lingine, ni kwa wale ambao wamepotea kutoka kanisani, mrudi kanisani mwenu na kuchukua ushirika wenu tena miongoni mwa waaminio; na halafu, pia, tungetaka kuwaleta wale waliorudi nyuma na kuondoka, warudi kwenye ushirika wa thamani wa kanisa tena, pamoja na watu.

¹⁴ Sasa, tutajaribu kutowaweka muda mrefu kila usiku. Usiku wa leo, ikiwa ni mara yangu ya kwanza hapa, labda, labda si watu watano ama sita hapa ambao nimewahi kuwaona maishani mwangu, ama waliowahi kuniona. Lakini mimi ni . . . Mwajua, usiku wa kwanza kwa kawaida huwa kidogo ni vigumu.

¹⁵ Unasema, “Unajua, sipendi jinsi mhubiri huyo anavyovaa tai yake.”

¹⁶ Vema, mke wangu hapendi, pia. Kwa hiyo mimi—mimi . . . Mwajua, na *kitu kingine* . . . Nilizoea kusema, “Jinsi alivyochana nywele zake,” lakini hilo si hoja sasa.

¹⁷ Na kwa hiyo sisi . . . Kitu fulani tu unachopaswa kukutana nacho, na kukutana na mtu huyo. Ndipo baada ya siku moja au mbili usiku, mnafahamiana, ndipo Roho Mtakatifu anaingia na kuanza kutubariki, na hayo yote madogo, mwajua, kama ninavyoyaita, misugvano midogo na wadudu wadogo

wamefagiliwa mbali. Ndipo basi tu—tuko tayari basi kuingia katika ibada. Nasi tuna siku kumi, Bwana akipenda, kwa hili, tunaomba ya kwamba litakuwa ni jambo kuu.

¹⁸ Sasa, si—si mkutano *wangu*, ni mkutano *wetu*, tuko pamoja. Na kila jitihada ndogo tunayoweza kutoa, hata kumzungumzia mtu fulani aje, kuagizia na kuwaleta maskini watu wagonjwa na kuwaingiza ndani wapate kuombewa, kumleta maskini mwenye dhambi, aliyepotea, waweze kuingia wapate kuokoka, kumleta asiyeamini aingie, aketi kitako na kuiangalia hii mikutano, labda huenda akabadilisha mtazamo wake.

¹⁹ Ku—kumbukeni tu, makafiri wengi mashuhuri wameongoka wakiisikiliza tu Injili. Unawezaje kuongoka usipoisikia Injili? Kwa sababu, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.”

²⁰ Na sasa tutafungua Neno hili la thamani, na kusoma kifungu kimoja kutoka Kwake, ama viwili, kwa ajili ya somo dogo, tupate muktadha. Ndipo ninaamini ya kwamba Billy alipaswa kusambaza kadi za maombi usiku wa leo. Mimi... Je, alifanya hivyo? Inueni mikono yenu kama kuna mtu yeyote aliye... Alifanya hivyo. Vema.

²¹ Wakati mwingine kwenye usiku wa kwanza, hatuwaombe wagonjwa. Tunaninii tu... Kamwe hatuna ratiba yoyote iliyowekwa wala kupangwa, tunamwacha tu Roho Mtakatifu aongoze. Nafikiri hilo ndilo watu wanalotaka, ni kumwacha tu Roho wa Bwana aongoze. Hatujui yale atakayotutaka tufanye. Lakini kama tutaendelea tu kuomba, tusile kupita kiasi, kula kidogo uwezavyo, na uombe, upige simu, umtafute mtu aje, hudhuria kila mkutano uwezao, nami nina hakika ya kwamba pamoja na jitihada hizo zote, Mungu atakutana nasi zaidi ya nusu uwanjani, ninaamini hilo.

²² Sasa, kabla tu hatujasoma Neno Lake, tunaamini *Hili* kuwa ni Neno la Mungu, tunaamini *Hili* kuwa ni Neno la kweli la Mungu. Kila kitu kilichoko *Hapa* ndani ni Neno la Mungu. Mnaamini hilo, kanisa lote? Hilo ni jema.

²³ Majuma machache tu yaliyopita, kulikuwa na mwuza mboga anayeishi kando ya njia kutoka mahali ninapoishi, naye ni mwaminio hodari sana, Mkatoliki, naye aliniambia, akasema, “Ndugu Branham, mara nyingi nimeshangaa ni kwa nini hukuwa Mkatoliki.”

Nami nikasema, “Mimi ni Mkatoliki.”

“Loo,” akasema, “Si—sielewi.”

Nikasema, “Naam, mimi ni Mkatoliki.”

Naye akasema, “Kamwe si—si—sikuoni kanisani mwetu, nawe una kanisa hapa chini,” basi kasema, “Kamwe si—si—sielewi hilo.”

²⁴ Nikasema, “Vema, ninataka kukuuliza: Je, ni kweli kwamba kanisa Katoliki linaamini ya kwamba Biblia hii ni historia ya kanisa Katoliki la mwanzoni, kwamba Yesu Kristo alianzisha kanisa Katoliki, Petro alikuwa ndiye papa wa kwanza, na kwamba Matendo Ya Mitume ni matendo ya kanisa Katoliki la mwanzoni?”

²⁵ Akasema, “Hiyo ni kweli kabisa.” Kwa sababu wengi wa watu wangu ni Wakatoliki, mimi ni Mwairishi na kwa namna fulani ninajua mafundisho ya—yao. Kwa hiyo, akasema, “Hiyo ni kweli.”

²⁶ Nikasema, “Vema, halafu sababu ya ninyi kutoishi kwa Biblia hii sasa, ni kwa sababu kwamba—kwamba papa ana ninii, kanisa, papa ana haki ya kubadilisha chochote atakacho katika Maandiko, kwa sababu alipewa haki ya kufanya hivyo, na hiki ni historia tu ya kanisa la kwanza.”

Akasema, “Naam, bwana.”

²⁷ Nikasema, “Vema, unaona,” nikasema, “ninaamini mimi ni Mkatoliki zaidi kuliko uliyo wewe.” Nikasema, “Kwa sababu wewe ni mmoja wa hawa Wakatoliki wa—wa siku mpya, wale wanaochukua fundisho la kanisa Katoliki siku hizi, nami ni Mkatoliki wa mtindo wa kale, ambaye anaamini yale Katoliki ya mtindo wa kale iliandika na kufanya.”

²⁸ Nikasema, “Hakika, wanapaswa kujua zaidi juu yake, walitembea pamoja na Bwana Yesu. Naye Petro, yule papa wa kwanza, alisema, ‘Hakuna mpatanishi mwingine kati ya Mungu na wanadamu, ila Mwanadamu Kristo Yesu.’” Nami nikasema, “Kwa namna fulani na—naamini hilo.” Kisha nikasema, “Ni—ninafundisha hasa kabisa kama kanisa Katoliki la mwanzoni lilivyofundisha, yale tu waliyoandika katika Biblia kuhusu yale waliyofanya.”

Akasema, “Ninaamini una kitu fulani, mwanangu.”

²⁹ Kwa hiyo hiyo ni kweli. Loo, ninalipenda tu Neno la Mungu, bila shaka ni Chakula kwetu kulisoma pamoja, kulisoma. Mimi si mwanatheolojia, sina elimu ya kuwa mwanatheolojia, wala sijaribu kuwa. Ninampenda tu Bwana Yesu, na kujaribu tu kutembea jinsi Yeye angenitaka nitembee, na kusema yale aliyoniamuru kusema, na kuwaombea wagonjwa. Naye amenibariki umbali huu, nami ninaamini atatubariki usiku wa leo.

³⁰ Sasa, kabla hatujalifungua Neno Lake la thamani, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, tunapozungumza na Mwandishi wake.

³¹ Baba yetu wa Mbinguni mwenye Neema, tunakuja Kwako tukiwa wanyenyekevu tu kadiri tujuavyo. Tunakuja tukikukaribia Wewe katika Jina la Mwanao mpendwa, Bwana Yesu, tukijua jambo hili, kwamba Yeye alisema, “Mwombeni

Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya.” Basi tunajua ya kwamba tuna haki ya kukukaribia Wewe, kuja kwa njia ya Jina Lake, kuja kwa njia ya msalaba, tukiomba rehema na msamaha wa dhambi na uponyaji kwa ajili ya miili yetu iliyo migonjwa, na kwa ajili ya neema ya Uwepo Wako, Bwana, katika mkutano huu, uendelee tu kuwa pamoja nasi usiku baada ya usiku.

³² Jalia mwanzo huu na uamsho huu uwe mwanzo tu wa uamsho wa mtindo wa kale ambao utatokea kwenye bonde hili, na kila kanisa, na miongoni mwa watu wote, kwamba watu watakuja kutoka juu ya milima hii kila mahali wapate kujifunza habari za Bwana. Tujalie, Bwana.

³³ Wabariki ndugu zetu wahudumu, hawa wanafunzi Wako waliotiwa mafuta, ambao wameshikilia ngome hapa, tukizileta kweli za Injili na kuzihubiri pasipo upendeleo wa wanadamu na kuitetea kweli. Na jinsi ambavyo umewabariki! Tunaomba ya kwamba mkutano huu utakuwa jiwe la kukanyagia kwao, Bwana, kwamba utawavuvia katika mkutano wao, na katika makanisa yao, na watu wao.

³⁴ Na ibada zitakapokwisha, jalia kusiwe na mmoja miongoni mwetu ila yule aliyempokea Roho Wako. Jalia kusiwe na mtu mmoja mnyonge anayetembea miongoni mwetu, bali Roho Mtakatifu na amponye kila mmoja. Tujalie, Bwana. Waite warudi kwenye ushirika wale ambao wamepotea, Baba Mungu.

³⁵ Ndipo tutakapoondoka usiku wa leo, kwenda kwenye makazi yetu tofauti kuanza siku mpya kesho, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani?” Tunajua ya kwamba alifanya jambo fulani mbele yao, kama tu alivyolifanya kabla ya kusulubiwa Kwake, hakuna mtu mwingine aliyewahi kufanya hivyo. Basi alipowaingiza ndani na kufunga mlango, ndipo akafanya jambo hili alilofanya hapo awali, nao wakatambua, upesi, ya kwamba ilikuwa ni Yeye.

³⁶ Mungu, tumeingia kwenye ukumbi huu wa shule usiku wa leo, ambao tunashukuru kwa ajili yake, tunaomba ya kwamba utabariki shule hii, na—na waalimu, na wakuu, na wadhamini, na wahusika wote, kwa sababu wamefungua milango kwa mkutano wa kidini.

³⁷ Nasi tumeingia, tuseme, na kuufungua ulimwengu nje, naomba uje miongoni mwetu, usiku wa leo, na ujifunue Mwenyewe jinsi ulivyofanya kabla hujasulubiwa, ndipo tutajua ya kwamba Wewe ni Bwana aliyefufuka. Itaimarisha imani yetu, Bwana, tutakupa Wewe sifa. Kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Mwokozi wetu, Bwana Yesu. Amina.

³⁸ Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake sasa. Ninataka tu kuchukua so—somo dogo la Maandiko, linalopatikana katika Yohana Mtakatifu mlango wa 12, kifungu cha 20:

Palikuwa na Wayunani kadha wa kadha... waliokwenda kuabudu kwenye sikukuu:

Basi hao walimwendea...Filipo, mtu wa Bethsaida... wakamwomba...mtu wa Galilaya, wakamwomba, wakisema, Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.

³⁹ Sasa, mada yetu ni hii, imekuwa yetu, mada yangu tangu nilipokuwa hapa hapo awali, ama, huko Oregon: “Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.” Hiyo inapatikana katika Waebrania 13:8, “Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.” Na sasa, juu ya haya yanayojulikana, na wengi wenu ninyi watu, Maandiko haya madogo: *Bwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu.*

⁴⁰ Huyu Myunani aliuliza swali hili. Alimjia Filipo, kwa mhudumu, naye akaomba amwone Bwana Yesu, ndipo akapewa na mhudumu wa Bwana Yesu majaliwa ya kumwona Bwana Yesu. Ndipo basi, kama Yesu ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kwa nini sisi wahudumu, basi, hatuwezi kuwaletea watu, ama watu kwa Bwana Yesu, kama tu vile Filipo alivyowaleta hawa Wayunani kwa Bwana Yesu? Kwa kuwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Sasa, ni—ni jambo la busara, na ni—ni la Kimaandiko, na ni la busara tu kama lilivyokuwa katika siku hiyo, *ikiwa* Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

⁴¹ Sasa, ninaamini ya kwamba Maandiko hayawezi kusema jambo lolote lisilo sahihi. Kuna mambo mengi katika Maandiko ambayo natamani tu ningaliweza, kwa imani ya kutosha, kuyafanya halisi kwa watu, lakini kamwe nisingeweza kumzuia mtu yeyote ambaye angeweza kufanya hivyo. Kama nisingeweza kutembea kama Henoko alasiri moja pamoja na Bwana, na niwe tu na furaha sana hata niende tu Nyumbani pamoja Naye, ni—nisingemzuia mtu yeyote ambaye alikuwa na imani kiasi hicho, ambaye angeweza tu kwenda Nyumbani pamoja Naye bila ya kufa, ama kuonja mauti katika ulimwengu huu.

⁴² Nasi tunajaribu leo, tunapoona wakati wa mwisho ukikaribia, kunapaswa kuwe na kuonekana kwa wakati wa mwisho kwa Bwana Yesu ambako Yeye alitabiri katika Maandiko, kwa sababu lolote alilosema, halina budi kutimia.

⁴³ Sasa, sisi wenyewe tuna kikomo, tunaweza kufanya makosa mengi, nami ninafanya zaidi ya wote, kwa sababu sisi tuna kikomo, bali Yeye hana kikomo, wala hawezi kufanya kosa. Sasa, ninaweza kuwaahidi jambo fulani, na kwa uwezo wangu wote naweza kusema, “Kweli ninamaanisha hilo,” halafu basi, ila nisiweze kutimiza yale niliyoahidi, kwa sababu hali za mambo zingebadilisha visa, lakini siyoy kwa Mungu, Yeye hawezi kutoa ahadi asiyoeweza kutimiza.

⁴⁴ Musa aliwazia jambo lile lile, ama Ibrahimu, hasa, “Hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini; bali alikuwa na

nguvu, akimtukuza Mungu; kwa kuwa alikuwa ameshawishika kabisa ya kwamba, yale Mungu aliyoahidi, Mungu angeweza kutimiza.” Kwa hiyo, Maandiko yote ambayo Mungu ametupa ni ahadi.

⁴⁵ Sasa, tunajishughulisha na kipengele cha kibinadamu cha kipengele cha wakati, na kitu pekee tunachojua ni inchi, futi, yadi, maili, kipimo, siku, majuma, saa, miezi, miaka, bali Mungu ni wa Milele, Yeye ni—Yeye ni. . . tuna nguvu iliyo na kikomo na akili iliyo na kikomo, bali Mungu hana kikomo katika mambo yote. Anajua mambo yote, alijua mambo yote kabla ulimwengu haujaanza, Yeye alijua mkutano huu ungekuwa hapa usiku wa leo, alijua mambo yote kabla hapajakuwapo na ulimwengu, maana Yeye angeweza kujua yale yangekuwa katika wakati wa mwisho tangu mwanzo, inamfanya Yeye Mungu. Hakuna kitu kingine, hakuna mwingine, hakuna kiumbe kingine, hakuna mtu mwingine angaliweza kufanya hivyo, ila Mungu pekee.

⁴⁶ Sasa, wakati mwingine tunashangaa ni kwa nini sisi. . . Yeye ni mkuu sana, na hata hivyo ni kwa nini hatumwoni zaidi ya vile tunavyomwona. Sasa, kama ningeshuka mjini usiku wa leo kwenye kila dhehebu la kanisa, nami ningesema, “Je, unaamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele?” kwa mchungaji wao mpendwa.

Angesema, “Hakika ninaamini.”

Ningesema, “Hilo ni sawa kabisa.” Vema basi, ningesema, “Je, unaamini kwamba Yeye angali ni Mwokozi yule yule aliyekuwa?”

Angesema, “Bila shaka, ninaamini hilo.”

“Je, unaamini ya kwamba Yeye yu hai leo kama alivyoishi wakati huo, ila tu katika umbo la utu wa Roho Mtakatifu?”

“Bila shaka, ninaamini hilo.”

⁴⁷ “Basi kama alikufa na kwa Damu Yake kuu, takatifu aliyoitoa pale Kalvari. . .” Ambayo haikuwa ya Kiyahudi, wala ya Mataifa, ilikuwa ni Damu ya Mungu. Damu hutoka kwa jinsia ya kiume, na katika kisa hiki Mwanaume alikuwa ni Mungu, akaumba Chembechembe ya Damu katika tumbo la uzazi la bikira aliyemzaa Mwana wa Mungu, ambapo Mungu alitandaza hema Lake na kufanya maskani pamoja na wanadamu, Imanueli.

⁴⁸ Sasa, kupitia Damu hiyo, Yeye alilitakasa Kanisa ili aweze kuendeleza kazi Yake, Mwenyewe akiishi katika Kanisa hilo, hiyo ndiyo Injili. Hilo linamfanya yule yule jana, leo, na hata milele. Sisi ni—ni— hatustahili kabisa baraka yoyote, hakuna kitu ambacho tungeweza kufanya kustahili hiyo, bali kwa neema isiyostahiliwa, Mungu alitupa majaliwa haya kuitwa watoto Wake, Wanawe na binti Zake, akitutakasa tunapokiri dhambi zetu, akiutakasa ulimwengu kutoka kwetu, kusudi apate

kutenda kazi Yake kupitia kwetu kwa Roho Mtakatifu kufanya na kuikusudia kazi Yake.

⁴⁹ Sasa, Yeye alisema wakati alipokuwa duniani, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya, na kubwa kuliko hii. . .” Tafsiri sahihi hapo ni *nyingi*; hakuna mtu angaliweza kufanya kubwa zaidi, bali Yeye angekuwa mahali pengi. Ndipo, Mungu alidhihirishwa katika Mtu mmoja, sasa Yeye amedhihirishwa katika Kanisa zima la ulimwengu mzima, kila mahali. Mungu anaweza kutenda kazi kupitia kila mwanamume na kila mwanamke ambaye ataufungua moyo wao, na kumwacha Bwana Yesu aingie na kufanya mapenzi Yake kupitia kwao.

⁵⁰ Sijali kama hata hujui ABC zako, kitu pekee unachopaswa kuwa nacho ni moyo mnyenyekevu, uliosalimishwa kwa Mungu, na Mungu atafanya mapenzi Yake kupitia kwako. Hiyo ni kweli.

⁵¹ Si lazima ujue mengi sana, inakubidi tu kumjua Mtu mmoja, huyo ni Bwana Yesu, kumjua Yeye ni Uzima. Huyu ndiye Mtu pekee unayepaswa kumjua upate kuwa na Uzima wa Milele. Kumjua Yeye, si kujua kile Kitabu, si kujua kanuni za imani, bali kumjua Yeye ni Uzima wa Milele, mjue Yeye kama Mwokozi wako binafsi, mjue Yeye kama Yule aliyekujaza na wema Wake na rehema Zake, ambaye ameondoa ulimwengu kutoka kwako, akautoa, akaupeleka mbali kama yule mbuzi wa Azazeli katika Agano la Kale uende nyikani ukauawe, usiweko tena.

⁵² Na kitu kile—kitu kile kile kilichokufanya utende dhambi na kufanya mambo uliyokuwa ukifanya kimeondolewa kwako kwa Damu Yake ya thamani iliyokutakasa na kukuweka kando kwa ajili ya utumishi Wake, ili kwamba aweze kufanya mapenzi Yake kupitia kwako, kufanya kazi kupitia kwako; rahisi tu, na, kuliadini.

⁵³ Sasa sisi, pia, tungeshikana mikono na mhudumu huyo, tukisema, “Tunaamini mambo haya.”

⁵⁴ Sasa, huenda nikamwambia mtu fulani huyu, “Je, unaamini ya kwamba Yeye ni yule yule kwa kila njia isipokuwa mwili wa kawaida, wa nyama?”

Angesema, “Vema, si—siamini kwamba Yeye angali anafanya miujiza.”

⁵⁵ Basi Yeye si yule yule, hana budi kuwa yule yule, Yeye ni Mwokozi tu leo kama alivyokuwa wakati huo, Yeye ni Mponyaji tu leo kama alivyokuwa wakati huo. Kwa kuwa nabii alisema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*,” mnaona, wakati uliopita.

⁵⁶ Siamini ya kwamba mwanadamu ana nguvu zozote za kichawi za kuwaponya watu. Ninaamini ya kwamba nguvu ziko ndani ya mtu binafsi anayeombewa, imani yao katika Kristo ndiyo inayoponya. Sasa, njia ya kwanza na ya neema sana ya njia yoyote ya kuponywa, ni kusikia Injili ikihubiriwa na

kuikubali. Hiyo ndiyo njia pekee ya kuwa, Injili ya wokovu, Injili ya ukombozi, Injili kamili, Injili kamili kwa ajili ya mtu mkamilifu, kwa ajili ya mwana mkamilifu, kwa ajili ya binti mkamilifu. Injili yote, yote aliyosema, yote aliyofanya, yote aliyohidi ni kwa kila mtu atakayeiamini. “Yeyote atakaye, na aje.” Methodisti, Baptisti, Pentekoste. . .

⁵⁷ Vema, Pentekoste, kamwe sijaninii. . . Nimekuwa, nilikuwa mhudumu wa Kibaptisti, mwajua, mimi ni Mbaptisti tu kadiri nilivyowahi kuwa. Pentekoste si dhehebu, Pentekoste ni tukio, ni tukio ambalo Mmethodisti, Mbaptisti, Mkatoliki, mtu yeyote anayetaka kulipokea amekaribishwa kuja kulipokea. Ni tukio, wala huwezi kuundia dhehebi tukio, ni—ni jambo ambalo Mungu amemfanyia mwanadamu. Mnaona? Naye atamfanyia mtu yeyote, haidhuru wewe ni wa kanisa gani.

⁵⁸ Sasa, katika hili, sasa, bila shaka, tunashirikiana na madhehebu, hilo ni sawa kabisa, kwa sababu hao ndugu wanakusanyika pamoja na—na kuunda madhehebu yao, ambalo ni sawa tu kabisa, hakika. Lakini ninamaanisha, sisi. . . Huwezi kusema, “Inakubidi kuja kwenye kanisa la Kipentekoste kabla hujapata hilo tukio.”

⁵⁹ Unaweza kulipokea huko nje shambani ukitaka, huko juu mwituni, huko chini pembeni mwa barabara. Popote pale, kanisa lolote ulilomo, kama ungali una njaa na kiu kwa ajili ya Kristo, Kristo yuko hapa kukuja kwa utimilifu wa nguvu Zake za Roho Wake. Hiyo ni kweli. Haidhuru uko wapi au wewe ni wa kanisa gani, ni kwa ajili yako.

⁶⁰ Sasa, kama Yeye ni yule yule, Yeye sio yule yule tu nusu au theluthi mbili ya yule yule, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Sasa, Neno Lake lilisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu,” ambapo hilo neno la Kiyunani hapo ni “kosmos” ambalo linamaanisha *utaratibu wa ulimwengu*, “hautaniona tena, bali ninyi mtaniona,” kanisa, “kwa kuwa Mimi,” na *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari. *Mimi* nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari.”

⁶¹ Mnaona kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka kwake kulivyokuwa? Kulikuwa ni kwa ajili ya kulisafisha na kulitakasa Kanisa, kuliweka kando, na kulijaza kwa nguvu Zake kuendeleza kazi zile zile alizofanya Yeye, ikimfanya Yeye yule yule jana, leo, na hata milele kuendelea zaidi na zaidi.

⁶² Sasa, njia pekee tutakayoweza kupata kutoka kwenye fungu hili, jambo tunalotaka kusema, ni kutafuta kujua kile alichokuwa jana, halafu hivyo ndivyo atakavyokuwa leo, na vile atakavyokuwa milele. Alikuwa ni Mtu wa aina gani?

⁶³ Tunapoona siku ikikaribia, inanifanya tu nitetemeke kutazama mitaani ninapopitia mijini na kuona na kusoma magazeti, na kusikia matangazo, na kadhalika, ya kulundikana

kwa dhambi, katika siku za kukaribia, na kukaribia zaidi wakati wote wa Kuja kwa Bwana. Lakini huwezi kufanya lolote juu yake, kwa sababu Mungu alisema ingekuwa hivyo tu.

⁶⁴ Ninaweza kutoa sauti kunena dhidi ya uovu, ni wajibu wetu kufanya hivyo, mimi na wewe tunapaswa kunena dhidi ya mabaya, uovu. Kamwe hatutaweza kuushinda na kuukomesha, ni wale tu walio na sikio la kusikia watakaoisikia, yeyote, “Wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu.”

⁶⁵ Sasa, basi tunapoona siku hii ikitokea, na kumwona Mungu akituma uamsho mkuu kote nchini, ninyi Wabaptisti: Billy Graham fulani; ninyi Wamethodisti: Jack Shuler fulani; ninyi Wapentekoste: Oral Roberts fulani. Mbona, yale Mungu amefanya! Ishara kuu, maajabu, miujiza imetendeka kote katika mataifa kila mahali, na daima taifa linagaagaa dhambini. Mnaamini hilo kuwa ni kweli? Mbona, liko moja kwa moja mbele ya macho yetu! Hakuna njia ya . . . Inaendelea kuwa mbaya zaidi wakati wote.

⁶⁶ Inanikumbusha juu ya hadithi moja ndogo, jambo dogo lililotukia, hasa, huko Louisville, Kentucky, yapata miezi sita iliyopita. Kulikuwa na mama aliyekuwa na mtoto wake mchanga, naye alikuwa katika, moja ya yale maduka ya bei rahisi huko Louisville, nao wakaanza kumwona maskini huyo dada, alikuwa, akachukua vifaa vidogo, mwajua, na kusema, “Angalia, Mpenzi! Angalia, Mpenzi!” Ndipo angeshikwa na wasiwasi na kukimbilia kaunta nyingine, aseme, “Angalia, Mpenzi! Angalia, Mpenzi!” Maskini mtoto huyo mchanga aliketi tu amekodoa macho, amekodoa macho.

⁶⁷ Kisha angeenda kwenye kaunta nyingine, na kaunta nyingine, akiingiwa na wasiwasi zaidi wakati wote. Hatimaye, akaokota maskini kengele ndogo, naye akaitikisa, na akasema, “Angalia, hii, Mpenzi!” Chochote kinapaswa kuvutia usikivu wa mvulana mdogo kama huyo, bali aliketi tu na kuangalia, akakodoa macho angani. Ndipo akaanguka kwenye kaunta na kuanza kupiga mayowe, akasema, “Loo, la! Haiwezekani kabisa!”

⁶⁸ Ndipo watu waliokuwa humo dukani, wakamwendea wapate kujua kulikuwa na shida gani. Naye akasema, “Mvulana wangu mdogo, yapata mwaka mmoja uliopita, alianza tu kukodoa macho angani.” Kisha kasema, “Nimefanya kila kitu, nimempeleka kwa daktari, naye daktari akasema alidhani alikuwa afadhali, lakini sivyo.” Halafu kasema, “Nimefanya tu yote niwezayo kuvutia usikivu wake kwa vidude vidogo vinavyopaswa kuvutia usikivu wa mvulana mdogo wa umri wake.”

⁶⁹ Kisha kasema, “Kitu hiki kidogo, mkokoteni mdogo wa farasi, ambao una kengele ndogo juu yake, kama mvulana mdogo

karibu na msimu wa Krismasi, namna hii, anapaswa kuwa akisikiliza kengele hizi ndogo kwenye theluji, na kadhalika,” kisha kasema, “naye anaketi tu na kukodoa macho angani,” kasema, “hana afueni.” Ndipo maskini moyo wake wa mama ukamlilia mtoto wake, kwa sababu alijua mtoto wake alikuwa na kasoro kiakili.

⁷⁰ Nafikiri hivyo ndivyo ilivyo na kanisa siku hizi, Mungu ametikisa karama ya kila namna, na kadhalika, ambazo angeweza mbele ya kanisa, nalo linaketi tu na kukodoa macho angani, “Vema, huo ulikuwa ni mkutano mzuri sana. Ndugu Roberts alikuwa na mkutano mzuri. Ndugu Billy Graham ana mahubiri mazuri.” Lakini hawasongi.

⁷¹ Tunachohitaji leo hii ni uamsho unaochangamsha nafsi, kitu ambacho kingeshuka na kusababisha mikutano ya maombi ya usiku kucha, wanaume na wanawake wakijiweka sawa na Mungu, na miji ikimgeukia Mungu, ishara kuu na maajabu yangeendelea tu kuongezeka.

⁷² Mungu hutuma karama Zake, Yeye huzitikisa mbele ya macho yetu, na kama tukizikataa, basi Mungu anaweza kufanya nini kuhusu jambo hilo? Kama mama huyo aliwazia hilo kuhusu mtoto wake mchanga, Mungu anawazia nini usiku wa leo kuhusu kanisa Lake wakati tumekuwa na mengi sana mbele zetu, watu mashuhuri nchini, Tommy Osborn, Ndugu Allen?

⁷³ Loo, ni watu wangapi mashuhuri wamevuka hili taifa mahali mahali? Kila namna za ishara na maajabu zimeonekana moja kwa moja katika wakati wa mwisho, na hata hivyo, kanisa linakaa limeduwaa, kasema, “Ulikuwa ni mzuri sana. Ni—ninaamini huenda nikahudhuria usiku mwingine, nione kitakachotukia kwenye mkutano unaofuata.”

⁷⁴ Hilo silo jambo la kufanya. Tunachohitaji tunapomwona Mungu akitenda kazi miongoni mwetu ni kuhusika nayo, kuomba na kupaza sauti, na kufanya yote tujuayo kufanya. Kuiacha Injili katika siku hizi za mwisho ivutie usikivu wetu.

⁷⁵ Biblia iliahidi ya kwamba Injili hii ingekuwa hivyo kila siku, kama vile katika siku za Luther, alifundisha utaka-... , ama, kuhesabiwa haki, ilifikia uchache wake wakati Yeye alipoingia katika wakati wa Methodisti ya Wesley kupitia utakaso, ndipo walipotulia kwenye hilo kanisa na ikawa ni hivyo tu, Mungu akainua Pentekoste, na sasa imefikia mahali ambapo Pentekoste inakuwa ya kawaida na isiyojali, Mungu anaendelea moja kwa moja, hiyo ni kusema, hatakoma hata kidogo, anasonga mbele moja kwa moja.

⁷⁶ Wana wa Israeli waliifuata Nguzo ya Moto, na kila wakati Moto huo uliposimama, walisimama pamoja Nao, na kama hawakusogea, waliachwa nyikani, iliwabidi kusogea mahali huo Moto uliposogea. Hivyo ndivyo Kanisa la Mungu linavyofanya daima, linatembea pamoja na ule Moto.

⁷⁷ Wakati Martin Luther alipouona ule Moto, matengenezo ya kwanza, alitoka kwenye kanisa Katoliki, naye akaunda dhehebu lake chini Yake. Huo Moto ukasonga ukaingia katika utakaso, tayari alikuwa ameunda madhehebu chini ya hayo wala asingeweza kusogea, kuendelea mbele zaidi. Wamethodisti waliuchukua, wakaunda madhehebu chini ya huo, wasingeweza kuendelea mbele zaidi; Pentekoste ilikuja na kuwanyang'anya.

⁷⁸ Sasa, tusipoangalia, huo Moto utasonga mbele moja kwa moja tena. Hebu na tukae chini ya huo Moto, tuabudu chini ya huo Moto, tuabudu katika nguvu za Roho, tukiliamini Neno la Mungu, tukiweka kando kila mzigo mzito, na kila dhambi ituzingayo kwa upesi.

⁷⁹ Na *dhambi* ni nini? Kutokuamini. “Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa.” Kuna dhambi mbili tu, moja... mambo mawili ulimwenguni: Moja ni imani, na hilo lingine ni kutokuamini. Kufanya uzinzi, kuvuta sigara, kunywa pombe, hizo si dhambi, hizo ni sifa za dhambi. Unafanya hivyo kwa sababu wewe si mwaminio, mwaminio hafanyi mambo hayo. Ama unaamini au huamini.

⁸⁰ Kuna matabaka matatu ya watu, kwa kawaida, yanayohudhuria mikutano mahali popote, na hao ni wasioamini, wanaojifanya waaminio, na waamini halisi. Nao daima ni umati huo, kila mahali. Na sasa kile tunachotaka kufanya ni kuwa waaminio halisi, kuitupa mioyo yetu katika Neno hili, na kuacha Neno liwe... Neno la Mungu liwe ndilo uamuzi wa mwisho wa kila mmoja wetu.

⁸¹ Unawajibika kwangu, unawajibika kwangu kama mhudumu, kama ukipata kuona jambo lolote linaloendelea katika mkutano ambalo haliambatani kabisa na Maandiko, basi unawajibika kwangu kuja kuniambia. Hiyo ni kweli, naam. Ninaamini ya kwamba Mungu hufanya mambo ambayo hayajaandikwa katika Biblia, ninaamini hilo; Mungu ni Mungu, Yeye anaweza kufanya atakalo. Lakini mradi tu ninajua linakaa mumo humo kwenye jalada lile pale, na ninajua ya kwamba Mungu alifanya ahadi, najisikia nina hakika nalo. Mradi tu ninaweza kuwa na hiyo, nitaridhika na chochote kile... kitu kingine chochote sisi... Hakuna kitu kingine kitakachoniridhisha namna hiyo, mradi tu ninaweza kudumu moja kwa moja na hilo.

⁸² Sasa, njia pekee ya kujua kile Yesu alicholeo leo ni kurudi nyuma na kutafuta kile alichokuwa jana, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Je, hilo lina mantiki? Je, hilo ni la busara? Vema sasa, hebu turudi nyuma basi.

⁸³ Nilikuwa nikisoma hapa dakika chache zilizopita katika Yohana Mtakatifu m—mlango wa 12, naamini ndivyo ilivyokuwa. Naam, bwana, mlango wa 12, na kifungu cha 20, cha 21. Sasa,

hebu turudi kwenye Kitabu cha kwanza cha Yohana Mtakatifu, nataka msome pamoja nami.

⁸⁴ Na kote katika hili juma, kusudi tusikae muda mrefu sana, nadhani mlisikia hiyo ikizimwa wakati huo, hiyo ilikuwa saa yangu, nina saa ya kengele kutoka Uswisi, nami nafikiri wakati nimesema ya kutosha, ni—ninaweka hiyo kengele, lakini sijaanza bado, kwa hiyo ilinibidi tu kuizima, hivyo tu.

⁸⁵ Sasa, Yesu Kristo yeye yule jana, leo na hata milele. Hebu tufungue mlango wa kwanza wa Yohana Mtakatifu na tuone. . . Kama ukisoma kitabu, nacho kilisema, “Mariamu na Yohana waliishi kwa furaha daima baadaye.” Mariamu na Yohana ni akina nani? Kamwe hutajua mpaka urudi kwenye sehemu ya kwanza ya kitabu na kukisoma kitabu hicho chote. Na kama Biblia inasema ya kwamba “Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele,” jinsi tu tutakavyoweza kujua kile alichokuwa. . . kile anachopaswa kuwa leo, itatubidi kurudi kuona kile alichokuwa jana. Hiyo ni kweli?

⁸⁶ Sasa, hebu tuone, tufungue Yohana Mtakatifu 1, tutanukuu tu Maandiko machache, ninawatakeni myasome. Nitapitia sura chache ndani yake usiku wa leo, kesho usiku nichukue mengine zaidi, na kadhalika, tunapoendelea, jinsi Roho Mtakatifu atakavyoongoza. Vema, hebu tuone kile alichokuwa jana, halafu kama tunaweza kuona kile hasa alichokuwa jana, na kumwona akija miongoni mwetu, na kufanya jambo lile lile leo, kila mgonjwa hapa ndani anapaswa kusimama na kumshukuru Mungu na kutoka nje, aseme, “Yote yamekwisha.”

⁸⁷ Sasa kumbukeni, kabla hatujalifikia, uponyaji wa Kiungu si maneno fulani ya kimazingaombwe ambayo mtu fulani anasema juu yako. Uponyaji wa Kiungu: kila mgonjwa hapa ndani tayari ameponywa machoni pa Mungu. “*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu.”

⁸⁸ Unasema, “Ndugu Branham, unamaanisha nini kwa hilo?”

⁸⁹ Vema, mtu fulani. . . Ningesema, “Ni wangapi waliokolewa miaka ishirini iliyopita?” Mikono mingi ingeinuliwa. “Ni wangapi waliokolewa miaka miwili iliyopita?” Mikono mingi ingeinuliwa.

⁹⁰ Vema, sikubaliani nawe, uliokolewa miaka elfu moja mia tisa iliyopita wakati Yesu alipokufa kwa ajili yako pale Kalvari, *uliukubali* tu miaka ishirini iliyopita na miaka miwili iliyopita. Unaona? Huo ndio wokovu wako, mpango umekwisha, Yesu alisema pale msalabani, “Imekwisha.” Mpango wote wa ukombozi wa mwanadamu ulikwisha, na kila baraka aliyohitaji katika safari ya maisha ilikamilishwa pale msalabani, kwa kuwa hapo “*Alijeruhiwa* kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa uovu wetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Unaamini hilo? Sasa, haya basi.

⁹¹ Sasa, tutarudi nyuma basi kushika kile alichokuwa. Sasa, tunaona katika Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, kulikuwa na jamaa mmoja jina lake Andrea. Tunajua kuhusu kuzaliwa Kwake, na—na kuhusu mahubiri Yake ya...kwenda nyikani apate kujaribiwa na ibilisi, na kisha baada ya siku arobaini, akatoka nje.

⁹² Na kulikuwa na mtu jina lake Andrea aliyeenda akamleta ndugu yake, Petro, na kumleta Simoni Petro, ambalo jina lake halikuwa hivyo wakati huo, na jina lake lilikuwa Simoni, bali si Petro, *Petro* linamaanisha “jiwe dogo,” kwa hiyo akamleta katika Uwepo wa Bwana Yesu. Huduma Yake ilikuwa changa sasa, Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza. Alimleta kwa Bwana Yesu, na mara Yesu alipomwalia, Yeye alisema, “Jina lako ni Simoni, na baba yako, wewe ni mwana wa Yona.” Hiyo ni kweli? “Jina lako ni Simoni, na jina la baba yako ni Yona.”

⁹³ Mvuvi huyu asiye na elimu, ambaye Maandiko yanasema kwamba alikuwa asiye na elimu wala maarifa. Hivi mlijua Biblia ilisema ya kwamba yule papa wa kwanza, kulingana na fundisho la kanisa Katoliki, alikuwa asiye na elimu wala maarifa? Biblia ilisema, “Alikuwa asiye na elimu wala maarifa.” Yohana Mtakatifu 4. Naye...Ninamaanisha Matendo mlango wa 4, samahani, naye alikuwa asiye na elimu wala maarifa, bali iliwabidi watambue alikuwa pamoja na Yesu.

⁹⁴ Na mara aliposema hivyo, upesi alimtambua kuwa ni Mwana wa Mungu. Kwa nini? Kwa nini aliitambua? Kwa sababu, kama kuna Wayahudi wowote humu ndani, mtajua hilo, msomaji yeyote wa Biblia atajua, ya kwamba Wayahudi walikuwa wakimtazamia Masihi kuja. Hiyo ni kweli? Musa alisema, “Bwana, Mungu wako atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.” Hiyo ni kweli? Nao walijua Masihi huyu angekuwa Mungu-Nabii ambaye angetoa ishara ya nabii kama Musa alivyokuwa, kwa kuwa huyo alikuwa ndiye nabii waliyekuwa wakimtazamia.

⁹⁵ Na wakati alipomwambia Simoni, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona,” upesi akatambua ya kwamba Huyu alikuwa ndiye Masihi waliyekuwa wakimtazamia.

⁹⁶ Tunaona siku chache baadaye, kulikuwa na jamaa mmoja jina lake Filipo, naye alikuwa na shauku sana, kweli alikutana na Kristo. Nami ninaamini bila shaka yoyote, ya kwamba mtu anapokutana na Kristo wakati mmoja, hawezi kuwa vivyo hivyo tena mradi tu angali hai. Kuna kitu fulani kumhusu Yeye ambacho ni tofauti na mtu mwingine yeyote, ama jamaa mwingine yeyote, ukiwahi kukutana Naye, ndipo utajua hujawahi kukutana na mtu kama huyo hapo awali.

⁹⁷ Si ajabu waliketi kitako, na kusema, “Mbona, kamwe hakuna mtu aliyepata kunena kama Mtu huyu!” Ukimsikia mara moja akinena, ile Sauti ndogo tulivu mo—moyoni mwako,

iliyomvutia nabii, hata moto na ngurumo na kadhalika havikumvutia, ila Sauti hiyo ndogo tulivu, aliufunika uso wake akaja mwishoni mwa hilo pango; ni kule kukutana na Kristo mara moja.

⁹⁸ Ndipo tunaona, angalieni, wakati Filipo alipopata kuwasiliana na Bwana Yesu, alihusika kuhusu marafiki zake wote. Kuna jambo fulani kumhusu, kwamba wakati wowote unapowasiliana Naye, anakubadilisha sana hata unataka kila mtu mwingine awe na ushirika huo mzuri sana, kuna jambo fulani kulihusu.

⁹⁹ Loo, linavutia na kuufanya moyo wako kutamani. Itakupeleka kwenye maeneo ya barafu ya kaskazini, ama kwenye misitu ya tropiki ya kusini katikati ya kila namna ya ibada za ibilisi, na kadhalika, kunyakua nafsi kutoka mikononi mwa adui, wakati wowote unapopata kile Kito cha thamani, Bwana Yesu Kristo.

¹⁰⁰ Upesi, alijua alikuwa na rafiki ambaye alikuwa, alikuwa wa kanisa la kiothodoksi, naye akatoka kwenda kumtafuta. Sasa, kama utaenda Palestina, utaona kwamba inachukua siku nzuri, kama maili kumi na tano kutembea kuzunguka milima, na kadhalika, kufika mahali Filipo alipoenda kumtafuta Nathanaeli.

¹⁰¹ Nami naweza kuwazia, hebu tuchukue safari ndogo na kumsikiliza kwa dakika moja, ninaweza kumwona akienda kwenye mlango wa Nathanaeli na kubisha mlangoni [Ndugu Branham aligonga mimbarani—Mh.], na—naye mkewe akaja mlangoni, anasema, “Vema, u hali gani?” Kasema, “Yuko wapi Ndugu Nathanaeli?”

“Vema, Ndugu Filipo, tuna furaha sana kukuona. Ninaamini yuko huko nje bustanini, alikuwa huko nje akiangalia shamba lake la mizeituni.”

¹⁰² Akapitia kwenye bustani ya matunda, naye akakuta, chini ya huo mtini kule nyuma, mtu amepiga magoti, akiomba. Bila shaka, yeye akiwa ni mwungwana Mkristo, alisimama kimya mpaka akamaliza kuomba. Ninawatakeni mwone, kamwe hakuruka juu na kumpa mkono, na kuuliza jinsi kila kitu kilivyokuwa kikiendelea. Mtu anapokutana na Yesu, moyo wake unawaka moto, hana wakati kwa ajili ya kitu kingine chochote ila Yesu, ndivyo ilivyo, hana budi tu kumwambia mtu fulani kulihusu. Angalieni, upesi akasema, “Njoo umwone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu!”

¹⁰³ Sio, “U hali gani?” au “Kila kitu kinaendeleaje? Je, mi—mitini inazaa vizuri mwaka huu?” Si...La, bwana, ujumbe ulikuwa wa dharura.

¹⁰⁴ Na kama ulikuwa wa dharura wakati huo, na sasa je? Kama ulikuwa ni wa dharura wakati huo tulipokuwa na miaka elfu mbili, bado, ya kuhubiriwa kwa Injili, na huu ndio wakati wa

mwisho, vema, ni zaidi sana jinsi gani leo? Mambo mengi mno ya kijamii, karamu nyingi kupita kiasi, mambo mengine mengi kupita kiasi mbali na Ujumbe halisi wa Bwana Yesu moja kwa moja hadi kwenye kiini. “Njoo uone nilichoona. Njoo upate ujuzi huu wa Roho Mtakatifu wa thamani ambaye amekuja maishani mwangu ambaye amenibadilisha, ambaye aliniongoa kutoka jinsi nilivyokuwa hadi jinsi nilivyo sasa.” Loo, jinsi tunavyoshukuru kwa ajili ya jambo hili!

¹⁰⁵ Alimkuta Nathanaeli chini ya mti huu, naye akasema, “Njoo umwone Yule niliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu!”

¹⁰⁶ Vema, ninaweza kumwazia huyu mwaminio mashuhuri, mwaminio wa kiorthodoksi akisimama, akipangusa vumbi kwenye vazi lake la Kipalestina, akitoa vumbi kutoka kwake, akasema, “Sasa, Filipo, najua wewe ni mtu mzuri, mwenye akili timamu, basi ni kitu gani hiki ambacho—ambacho unaniambia? ‘Njoo umwone Yesu wa Nazareti’? Je, neno lolote jema laweza kutoka Nazareti?”

¹⁰⁷ Vema, nafikiri Filipo alimpa jibu zuri sana nililopata kusikia maishani mwangu, akasema, “Njoo, uone.”

¹⁰⁸ Hilo ndilo wazo. Usikae nyumbani na kukosoa, njoo, ujionee mwenyewe. “Yachunguzeni Maandiko, ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele, na Hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi,” alisema Bwana Yesu.

¹⁰⁹ Sasa, yeye alisema, “Njoo, uone.”

¹¹⁰ Ninaweza kuwazia walipokuwa wakienda zao barabarani, vema, alikuwa tayari kwenda, loo, ninaweza kumsikia akisimulia kuhusu kumwona Roho Mtakatifu akimjia Bwana Yesu kwenye ubatizo, jinsi alivyotoka kwenda nyikani, “Mbona,” akasema, “wakati ilipoanza, ilikuwa tu ni ile Nguzo ya Moto iliyokuwa ikiwafuata wana wa Israeli tulipokuwa tukija katika nchi hii; ndipo basi ilipokaribia, ilionekana kama hua; halafu jambo la pili, ilikuwa katika mifano mitatu mbalimbali; kisha ikashuka ndani Yake, na Sauti ikanena, ikisema, ‘Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa Naye.’”

¹¹¹ Ndipo ninaweza kumsikia akisema, “Je, unamjua maskini yule mvuvi ambaye tulienda kununua wale samaki kutoka kwake wakati ule, naye alikuwa hajui kusoma na kuandika, asingeweza kuandika jina lake kwenye ri—risiti, kwamba ulitaka risiti?”

“Naam, ninaikumbuka.”

¹¹² “Mbona, jana tu kabla sijaondoka, mbona, alikuja mbele za Bwana Yesu, ndugu yake alienda akamchukua, na kwa hiyo akamleta hapa, ndipo alipomwona Petro, ama, Simoni, Yeye alisema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’ Loo,

haingenishangaza, Nathanaeli, lakini utakapoenda mbele Zake, Yeye atasema, 'Jina lako ni Nathanaeli.'

¹¹³ "Loo sasa, hebu kidogo tu sasa, Filipino, kidogo unakiuka mipaka na hilo. Kamwe hatasoma mawazo yangu, mimi ni—mimi ni mmoja wa wale watu wenye akili thabiti, ka—kamwe hatasoma mawazo yangu. Kamwe sitaamini hilo."

¹¹⁴ Vema, anakuja mpaka anafika Mbele za Bwana Yesu. Hapana shaka mara tu alipomsikia akinena, Mtu huyo alizungumza tofauti na mtu yeyote aliyewahi kumsikia, alinena kwa mamlaka, alijua alichokuwa akizungumzia.

¹¹⁵ Kwa hiyo, Yeye akasema, akisimama akinena, ama katika mstari wa maombi, ama hali yoyote aliyokuwamo wakati Filipino na Nathanaeli walipopanda pale, Yesu aligeuza macho Yake na kuliangalia kusanyiko, na mstarini, popote pale, na kusema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!"

¹¹⁶ Vema, mkosoaji fulani anaweza kusema, "Hakika Yeye alijua alikuwa ni Mwisraeli, walikuwa Palestina."

¹¹⁷ Kulikuwa na Wayunani, kulikuwa na Waarabu. Wote walikuwa... Wote walikuwa wamevaa vazi la mashariki, si jinsi alivyokuwa amevalia, si rangi yake ya hudhurungi, isingelela tofauti yoyote. Lakini Yesu alijua ya kwamba alikuwa ni mwaminio wa kiothodoksi, Yeye alisema, "Tazama Mwisraeli, ambaye hamna hila ndani yake!"

¹¹⁸ Sasa Filipino... Nathanaeli alikuwa ni mwanachuoni aliyefunzwa vizuri, kwa hiyo akasema, "Rabi," ambalo linamaanisha *mwalimu*, "ulinijua lini Wewe? Ulijuaje kwamba nilikuwa m—m—mtu asiye na hila?" Ningesema leo mtu mwaminifu, mwema. "Ulijuaje hilo?"

¹¹⁹ Akasema, "Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona." Huyo alikuwa ni Yesu jana, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, huyo ni Yesu leo.

¹²⁰ Mnajua yale Filipino aliyosema wakati Yeye, ninamaanisha, Nathanaeli aliyosema wakati alipofanya jambo hili? Alisema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli."

Yesu akamwambia, "Kwa sababu nimekwambia hivi, unaamini? Basi utaona mambo makuu kuliko haya."

¹²¹ Mnalipata? Hilo hapo. Mnaona? Aliliamini, kwa sababu alijua ya kwamba Masihi angekuwa ni Mungu-Nabii, Mtu aliyesimama na angetabiri na angeweza kubashiri na angeweza kuona kimbele, na kusema kimbele, pia Yeye angekuwa Imanueli.

¹²² Akasema, "Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli." Aliliamini, naye, jina lake halipatikani na mauti miongoni mwa wanadamu usiku wa leo na nafsi yake haifi pamoja na Mungu. Ataishi milele, kwa sababu alitambua

jambo hilo hapo mwanzo, na kusema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu.”

¹²³ Sasa, bila shaka kulikuwa na wale waliosimama karibu ambao hawakuamini hilo, kulikuwako na makuhani wengi waliokuwa wamesimama karibu, watu mashuhuri, watu wa kidini, watu wema waliosimama karibu, nao iliwabidi kuwajibika kwa kusanyiko lao. Walijua jambo hilo lilikuwa likifanywa, na hilo lilikuwa ni mwujiza mkubwa zaidi kuliko kuwaponya wagonjwa, kwa sababu huenda ikawa wagonjwa wangepewa kuamka, lakini hiyo isingewezekana, ilibidi iwe ni nguvu fulani za kimbinguni.

¹²⁴ Kwa hiyo, badala ya kujaribu kulielezea, mnajua walichofanya? Walilihesabu tu kama ibilisi, nao wakasema, “Yeye ni Beelzebuli, mkuu wa pepo, anafanya ishara hizi kupitia huyo.” Beelzebuli, mpiga ramli, na mtu yeyote anajua ya kwamba kupiga ramli ni kwa ibilisi; huyo ni ibilisi na kazi za ibilisi. Vema. Kwa hiyo akasema, “Yeye ni ibilisi.”

¹²⁵ Yesu akageuka, na kusema, “Mkisema hivyo dhidi Yangu, Mwana wa Adamu, nitawasamehe hilo. Lakini,” vinginevyo namna hii, “siku yaja ambapo Roho Mtakatifu atakuja, Naye atafanya jambo lile lile, na yeyote atakayesema neno moja dhidi Yake, hatasamehewa kamwe, katika ulimwengu huu, wala katika ulimwengu ujao.” Mnaona? Lilikuwa ni jipya kwao wakati huo. Sasa, Kristo amekufa, sasa Roho Mtakatifu yupo hapa.

¹²⁶ Halafu, soma kifungu kinachofuata: “Kwa sababu wanamwita Roho wa Mungu roho mchafu,” walimwita Roho wa Mungu Ambaye alijua mambo hayo naye alikuwa akiyafunua kwa siri za moyo, kama vile Mungu-Nabii alivyopaswa kufanya, walisema, “Yeye ni mtu mwovu. Ni roho mwovu ndani yake, namna fulani ya Beelzebuli, ibilisi, aliye ndani Yake anayesoma mawazo ya watu hao, huyo ndiye anayefanya hivyo.”

¹²⁷ Loo, ni dhambi mbaya jinsi gani: kutokuamini! Mbona, watu hao, hakukuwa na kitu dhidi ya maisha yao, walikuwa watakatifu, makuhani tu katika ukoo wa makuhani. Ilibidi wawe ni Walawi, iliwabidi wazaliwe namna fulani, baba yao, babu yao, na baba wa babu yao huko nyuma ilibidi wawe ni makuhani. Walijua torati, walijua Neno herufi kwa herufi hasa, waliishi ndani yake mchana na usiku tangu utotoni na kuendelea, hakuna mtu angaliweza kuyagusia maisha yao, na hata hivyo, Yesu alisema, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi,” kwa sababu hawakuamini walipoiona kazi ya Mungu ikiendelea. Wao...

¹²⁸ Aliwahukumu, kwa sababu kwamba hawakuamini. Jambo baya zaidi lililopo ni kutokumwamini Mungu; hiyo ndiyo dhambi pekee iliyopo, kutokuamini, kutokuliamini.

¹²⁹ Sasa, tunaona. . . Hebu twende pamoja naye mbele kidogo. Hebu na tufungue sasa, hayo ni Matendo, uh, Yohana Mtakatifu mlango wa kwanza, wa pili, hebu twende katika Yohana Mtakatifu mlango wa 4.

¹³⁰ Sasa, kulikuwako na matabaka matatu ya watu ulimwenguni wakati huo, kuna matabaka matatu ya watu, vizazi vitatu vya watu, ama matabaka ya watu, hasa, ulimwenguni siku hizi, nayo yalitokana na wale wana watatu wa Nuhu. Kama tunaamini Biblia, ulimwengu mzima, vizazi, watu wote ulimwenguni, walitokana na hao watoto watatu, Hamu, Shemu, na Yafethi, hao wana watatu: Myahudi, Mmataifa, na Msamaria.

¹³¹ Sasa, Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi, pia. Na Masihi ajapo, Yeye huwajia wale wanaomtazamia. Mnaamini hilo? Ninaamini atakapokuja kwa ajili ya Kanisa Lake, atakuja kwenye Kanisa linalomtazamia Yeye kuja. Sasa, msiache lilingane na hilo, "Alikuwa kwa walio Wake, walio Wake hawakumpokea." Lakini basi, alikuwa amejitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi kwa kufanya ishara hii maalum, hata wakajua ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi.

¹³² Sasa, Yeye alikuwa na haja ya kupitia Samaria. Samaria ilikuwa ninii. . . Mwajua, ninyi, wahudumu na wasomaji wa Biblia mnajua jinsi jamii ya Wasamaria ilivyoibuka. Sasa, tunaona ya kwamba walikuwa wakimtazamia Masihi, pia. Naye Yesu akaja kisimani pale, Sikari, na yapata adhuhuri akawatuma wanafunzi Wake waende wakanunue chakula.

¹³³ Basi alitokea mwanamke mmoja, hebu tuwazie kwamba alikuwa ni mwanamke mwenye sifa mbaya, naye alikuwa akiishi na mume wake wa sita, naye akaja kisimani kuchota maji. Hapana shaka mchungaji wenu amehubiri juu yake mara nyingi, bali ninajaribu kusema kile alichokuwa jana, ili mweze kuona kile angekuwa leo.

¹³⁴ Sasa, Yeye amejitambulisha Mwenyewe kwa Wayahudi. Tutafikia mahali pengine pengi baadaye, lakini ili tu kugusia jambo hilo. Katika dakika chache tutafanyiza mstari wa maombi.

¹³⁵ Sasa, Yeye anamjia mwanamke huyu, ama mwanamke huyu anakuja kuteka maji, hasa, na ni yapata adhuhuri, nami ninaweza kumwona akitoka huku nywele za—zake zikining'inia chini, hazijachanwa. Naye alikuwa na ule—ule mtungi begani mwake, kama wanawake wa mashariki wanavyoubeba kwa kawaida.

¹³⁶ Wanaweza kuweka galoni tano za maji juu ya kichwa chao, galoni tano kwenye nyonga, na galoni tano *hapa*, wanatembea wakizungumziana, pasipo kumwaga tone hata moja, kwa usawa kamili.

¹³⁷ Naye mwanamke huyu labda alikuwa na mtungi huu wa maji. Hebu tuone, huenda alikuwa, kwa sababu alikuwa

ametoka usiku kucha na ndio kwanza aingie, sababu ya yeye kuwa . . . ama alilala kupita kiasi. Huenda ilikuwa ni kwa sababu hangeweza kuja kisimani pamoja na wanawake waadilifu. Kulikuwa na ubaguzi mkubwa miongoni mwa hao katika siku hizo, mwanamke mchafu asingeweza kuchangamana na—na wanawake safi.

¹³⁸ Kwa hiyo kwa vyovyote vile, alikuwa kisimani. Naye Yesu . . . Kwa namna fulani ni mandhari, kile kisima kule Sikari, kitu kama hiki, mizabibu ilikulia ukutani, na kile kisima cha mjini pale ambapo watu walikuja kuchota maji yao. Ninaweza kumwona huyo mwanamke akija, akichukua ile mipini miwili mikubwa, na kuweka kulabu ndani yake, na kushusha winchi achote maji. Ndipo akasikia Sauti ikisema, “Mwanamke, nipe maji ninywe.”

¹³⁹ Ndipo akatazama, akamwona Mwanamume Myahudi mwenye umri wa makamu, ameketi ameegemea kile kisima. Labda alionekana mzee kidogo kuliko vile alivyokuwa hasa, ninaamini alipokuwa na yapata miaka thelathini, walimwambia ya kwamba alionekana mwenye umri wa miaka hamsini.

¹⁴⁰ Wakasema, “Wewe hujapata bado zaidi ya miaka hamsini, nawe unasema ya kwamba umemwona Ibrahimu?”

Akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.”

¹⁴¹ Kwa hiyo wao—wao . . . Lakini alionekana mwenye umri wa miaka hamsini alipokuwa na umri wa miaka thelathini tu. Na kwa hiyo huenda alionekana amezeeka kidogo ameketi kule nyuma, labda mchirizi mdogo wa mvi katika nywele Zake ama ndevu, kwa sababu ule mzigo mkubwa, dhambi za ulimwengu ziliwekwa mabegani Mwake. Naye huyo hapo ameketi pale.

¹⁴² Alimwona Myahudi huyu. Nao walikuwa na ubaguzi siku hizo, kama tu ilivyokuwa kaskazini na kusini kati ya wa—watu weupe na watu weusi. Lakini, ndipo akasema, “Si kawaida kweni Wayahudi kumwomba mwanamke Msamaria kitu kama hicho.” Kasema, “Ha—hatuna uhusiano sisi kwa sisi.”

¹⁴³ Sikilizeni ile Sauti ikirudi: “Mwanamke, kama ungalijua ni Nani anayesema nawe, ungeniomba Mimi maji unywe; ningekupa Maji usije hapa kuchota.”

Naye akasema, “Kisima ni kirefu, wala huna kitu cha kuchotea.”

¹⁴⁴ Mazungumzo yakaendelea kuhusu kuabudu katika mlima *huu*, huko Yerusalemu, na kadhalika. Baada ya kitambo kidogo, Yesu akisimama pale, alikuwa na haja ya kupitia, Baba alimtuma kule, na halafu Yeye hakujuua kile kingetukia, angekuwa anafanya nini? Alikuwa akijaribu kujua shida ya mwanamke huyo ilikuwa ni nini. Alipopata shida yake, ni wangapi wanaojua ilikuwa ni nini? Hakika, alikuwa akiishi

katika dhambi. Na Yeye, Yeye alisema nini? “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

Akasema, “Sina mume.”

Akasema, “Umesema vema, kwa kuwa umekuwa na waume watano, na kwa hiyo, yule unayeishi naye sasa siye mume wako.”

¹⁴⁵ Sasa, hivi alisema, “Mtu huyo ni Beelzebuli”? La, bwana. Hivi yeye alisema, “Yeye ni . . . Lazima ana kasoro, hana budi ana u—ugonjwa mbaya sana wa telepathia ya kiakili”? La, bwana. Alijua mengi zaidi kumhusu Mungu kuliko nusu ya huduma ijuavyo siku hizi. Hiyo ni kweli.

¹⁴⁶ Akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii.” Amina. “Naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya, lakini u Nani Wewe?”

¹⁴⁷ Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.” Inasikitisha sana kwamba hatujui jambo lile lile, sivyo? Hiyo ni kweli.

¹⁴⁸ Akasema, “Tunajua, sisi Wasamaria tunajua ya kwamba Masihi huyo atakapokuja, Yeye atakuwa ni Mungu-Nabii, Yeye atatuambia mambo haya.” Alifundishwa, angali katika dhambi zake, alijua cha kutazamia alipokiona. Naye akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii, nami najua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe Ndiye.”

¹⁴⁹ Ndipo akaangusha mtungi wake wa maji na kukimbia mjini. Msikilizeni: “Njoni mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Nayo Biblia ilisema ya kwamba watu wa mji huo walimwamini kwa sababu ya neno la yule mwanamke. Loo, jamani!

¹⁵⁰ Huyu alikuwa ni Yesu jana, hivyo ndivyo Yesu alivyojitambulisha Mwenyewe. Kamwe hata wakati mmoja hakujiwakilisha Mwenyewe miongoni mwa Mataifa namna hiyo. Kwa nini? Mataifa hawakuwa wakimtazamia. Mataifa, tulibeba rungu begani mwetu, tukitumikia sanamu katika siku hizo, bali Yahudi walikuwa wakimtazamia Masihi, nao Wasamaria walikuwa wakimtazamia Masihi. Lakini tumekuwa na miaka elfu mbili ya ulimwengu wa kanisa, nasi tunamtazamia Masihi katika siku za mwisho. Je, ulijua Yeye aliahidi angefanya jambo lile lile? Tatalifikia baadaye juma hili. Nitawapa moja sasa hivi.

¹⁵¹ Yesu alisema Mle ndani, kabla tu hatujafunga, Yesu alisema katika Maandiko, wakati anaposimulia juu ya Kuja kwa . . . Kuja Kwake mara ya Pili, bahari ikivuma, mawimbi, na kadhalika, mambo yakitukia, ishara kuu zingekuwa zikitukia, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

¹⁵² Hivi mliona wakati aliposema katika siku za Nuhu, aliorodhesha yale waliyokuwa wakifanya, ili kwamba akili ya kiroho iweze kuichukua? Ameyaficha kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili. Yafungueni macho yenu ya kiroho sasa, ufungueni ufahamu wenu wa kiroho. Alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, walikuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa.” Lakini Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

¹⁵³ Sasa angalia, daima tumekuwa na matabaka matatu ya watu, jamii tatu za watu, hatua tatu mbalimbali za watu, angalieni, huyo hapo Msodoma mwenye dhambi ambaye hakuijali; huyo hapo Lutu, yule mshiriki vuguvugu wa kanisa kule chini akihubiri katika Sodoma; na huyo hapo Ibrahimu, aliyeitwa atoke na Mteule. Ninajisikia kubarikiwa sasa hivi. Angalieni, wote walioitwa watoke, watu waliotengwa... *Kanisa* linamaanisha, “waliotengwa, walioitwa kutoka ulimwenguni.”

¹⁵⁴ Kulikuwako na Ibrahimu, aliyeitwa atoke, akiwa na maisha magumu, akiteswa, akadhihakiwa, ameketi huko nyikani kwenye ardhi kame kwenye kivuli cha mwaloni. Lakini saa ya Ujumbe ilipofika, aliangalia nje wakati wa hari, naye akawaona watu watatu wakija, wamejaa mavumbi nguoni mwao, ndipo Ibrahimu akaangalia tena, akijua kulikuwa tu na *kitu fulani* juu yake. Mtoto halisi wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili anajua Roho wa Mungu anapopiga. Naam, bwana. “Kondoo wangu wanaijua Sauti Yangu.”

¹⁵⁵ Ibrahimu akaangalia upesi sana, akatoka akaenda mahali walipokuwa, na kusema, “Geukeni, njoni, mkaketi chini ya mwaloni kidogo, na hebu...mpumzike. Nami nitaleta maji kidogo mkanawe miguu yenu, kisha nitawapa kipande cha mkate, kisha mwendele.”

¹⁵⁶ Vema, wakaja na kuketi chini, wageni kutoka Nchi ya kigeni. Loo, hakika, *mbali* sana! Nao wakaketi chini ya mti, akaingia mbio hemani, hebu na tuyaingilie mazungumzo yao, “Sara, kipenzi, hakika tu kama ninavyosimama hapo, Huyo hapo amesimama moja kwa moja hapo nje. Nenda upesi sana na uanze kuandaa chakula hiki, uchekeche vizuri sana, na uuwekelee vizuri mekoni pale, nataka upike keki kadhaa.”

¹⁵⁷ Akakimbia nje, akatafuta pande zote, akachukua maskini ndama aliyenona kabisa aliyeweza kumpata, akamchinja, kisha akamtengeneza, kisha akatoka na kuwalisha nyama, na maziwa, na ugali. Nami ninaweza kumwona mzee Ibrahimu akiwa na mgwisho wa inzi, mwajua, tuseme akiwafukuza nzi. Ni Wakentaki wangapi walio hapa ndani, wanaojua—wanaojua mgwisho wa nzi ni nini? La, niko mbali sana na nyumbani. Loo, la, mimi si, la, la, hilo ni sawa.

158 Naam, bwana. Vema, nimesimama mara nyingi mezani pamoja na ninii—ninii. . . Mama alikuwa akitengeneza kitu cha karatasi kwenye kijiti wakati nisingeweza kupata mgwisho wa kijani kibichi, mwajua, na kuwawafukuza nzi wakati hatukuwa na skrini, maskini mlango mdogo wa kibanda, wala hakuna sakafu kwenye kitu hicho. Na maskini kitanda kidogo tu pembeni kilichotengenezwa kwa makapi, na, mbona, bila shaka, makapi ya mahindi. Nilimwona baba yangu akiwa na brashi ya kunyolea ya kapi la mahindi namna *hiyo*, kuchukua hayo makapi ya mahindi kwa ajili ya kufanya brashi ya kunyolea. Tuliishi maisha magumu.

159 Na huko nyuma katika siku hizo, ninaweza kumwona Ibrahimu amesimama pale, akiangalia, mwajua, kuna *kitu fulani*. Wala wanawake hawakuwa washupavu kama walivyo siku hizi, walikaa nyuma na kushughulikia kazi zao siku hizo, kwa hiyo alikuwa amerudi nyuma hemani. Siku hizi, hana budi kuendesha shughuli za mumewe, na shughuli zingine zote, na kadhalika. Lakini siwaambii hayo ninyi akina dada, bila shaka nyote hamfanyi hivyo, bali—bali ninazungumza juu ya wanawake wa ulimwengu. Kwa hiyo, Sara, alikaa mahali pake huko nyuma hemani.

160 Ibrahimu akasema. . . akaanza kuona Mmoja wao akianza kuangalia upande wa Sodoma, alijua jambo fulani litatendeka. Wawili wao wakasimama. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . hawa wawili kuleta ujumbe, Billy Graham wa kisasa, kama aliwahi kuwako, kuhubiri toba.

161 Na toba sikuzote. . . La, hakuna miujiza, ila tu kuwapofusha watu, nako kuhubiriwa kwa Injili humpofusha asiyeamini, hiyo ni kweli kabisa. Huyu hapo chini kule, akihubiri, akaenda kanisani, kwa—kwa Lutu, na pamoja na Lutu, akajaribu kuleta imani kwa hilo. . . Mbona, kule kupofushwa kwao, wangali walipapasa-papasa usiku kucha kuwatafuta, kuwatafuta watu hawa. Walichafuliwa kabisa, kama waliwahi kuchafuliwa.

162 Sasa, mwangalieni Huyu aliyebaki nyuma, sasa, huo ndio Ujumbe. Kanisa la kawaida leo limekuwa na ujumbe wake kupitia kwa akina Billy Graham, na—na watu mashuhuri wa dhehebu hilo, wamekuwa na ujumbe wao wa “Tokeni Babeli,” bali hawatausikiliza, si zaidi ya walivyofanya huko nyuma katika siku hiyo.

163 Lakini sasa ngoja, kulikuwa na Malaika aliyebaki, Mmoja wao alibaki nyuma. Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Mmoja wao alibaki nyuma na Ibrahimu, lile Kanisa teule. Hebu tuone kile alichofanya, Yeye kamwe hakuwaita watubu. Hebu tuone yale aliyofanya, Yesu alisema jambo lile lile lingejirudia. Nami nawatakeni mwone, baada ya Malaika huyu kufanya yale aliyofanya, na akaondolewa kutoka—kutoka machoni pa Ibrahimu, Ibrahimu. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

164 ...mwili, akionyesha kimbele yale angefanya katika mwili wa Kanisa Lake katika siku za mwisho. “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Mungu, akiishi katika mwili wa Kanisa Lake. Akifanya nini? Yale aliyofanya kule, yale aliyofanya alipokuja duniani. Mwangalieni, Yeye alifanya nini?

165 Aliketi pale, akamwangalia Ibrahimu, Biblia ilisema mgongo Wake ulikuwa umeelekezwa kwenye hema, akasema, “Ibrahimu, yu wapi Sara, mkeo?” Uliwahi kulisoma? “Yu wapi Sara, mkeo?”

166 Alijuaje alikuwa ameo? Kisha alijuaje alikuwa na mke? Halafu alijuaje jina lake lilikuwa Sara? Hiyo ilikuwa telepathia ya namna gani?

167 Ndipo Ibrahimu akasema, “Yuko hemani nyuma Yako.”

168 Ndipo basi yule Malaika akasema, “Nitakuzuru kulingana na muhula wake.” Kama tujuavyo, zile siku ishirini na nane. Kasema, “Mimi...” Sara alikuwa ni mwanamke mkongwe. Kasema, “Nitakuzuru kulingana na muhula wake, nawe utampata huyu mtoto, kwa Sara, ambaye nilisema mtampata. Nitatimiza ahadi Yangu.”

Naye Sara, akiwa hemani nyuma Yake, akacheka kimoyomoyo. Hiyo ni kweli? Naye huyo Malaika akiangalia *huku*, kasema, “Kwa nini Sara akacheka?”

169 “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Atakuja kwa Kanisa la Mataifa. Mataifa hawakuwa nalo katika wakati wowote mpaka wakati huu, ndilo hili leo. Ni kitu gani? Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele, Yesu Kristo, Bwana Yesu yeye—yeye yule, akiwa na ishara zile zile, Roho Mtakatifu yeye yule akiishi Kanisani siku hizi, akifanya mambo yale yale aliyofanya.

170 Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 14, ninaamini yapata kifungu cha 8, Yeye alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.”

171 Sasa, tunaona kile alichokuwa jana, hivyo ndivyo alivyokuwa. Walimwamini, kwa sababu Yeye alikuwa ndiye Masihi, alithibitishwa kuwa ndiye Masihi. Sasa, kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, itambidi kufanya vivyo hivyo wakati wa kumalizia kwa wakati huu wa Mataifa, kama tu alivyofanya wakati wa kumalizia kwa wakati wa Wayahudi na Wasamaria. Asipofanya hivyo, basi alifanya jambo fulani kwa ajili yao ambalo hakutufanyia, basi asingekuwa mwenye haki.

172 Yeye hana kikomo, hawezi kubadilisha mipango Yake. Na kama Mungu akituruhusu kuja katika Uwepo Wake, wakati huu wa Mataifa, bila kufanya na kutuonyesha vile vile alivyowafanyia huko nyuma, basi amefanya jambo ambalo

hakutufanyia sisi, lakini Yeye hajaturuhusu kufanya hivyo. Tuko hapa kwenye ile saa leo hii ambapo Yesu Kristo yu hai. Amefufuka katika wafu, hajafa, yu hai apate kutenda kazi, na kufanya vile vile kama alivyofanya jana Kanisani Mwake ambalo litajisalimisha Lenyewe na kumwacha Roho Mtakatifu atende kazi.

¹⁷³ Ninyi Wapentekoste, wengi wenu, juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, pamoja na kunena kwa lugha mmetoa jumbe, na mambo hayo yote, hivyo ndivyo Biblia inavyofundisha hasa, hiyo ni kweli kabisa, mlitoa unabii, na kadhalika. Basi kwa nini sisi, tunapoona hili limeanza kushuka sasa, tumetulia juu ya hilo . . . ?

¹⁷⁴ Mungu huliinua Kanisa Lake juu zaidi kidogo, juu zaidi kidogo, kama tu piramidi, inapofika kileleni, hatimaye kufikia kwenye kilele. Mliona, ile piramidi ilikataliwa? Lile jiwe lililowekwa juu ya ile piramidi kuu, kama uliwahi kuwa Misri, kamwe halikuifunika. Kwa nini? Hilo jiwe la kichwani lilikataliwa. Basi angalia jiwe hilo, kila jiwe, linapofikia mwisho wake, ilibidi lichongwe kwa utaratibu sana kwa ajili ya jiwe la kichwani.

¹⁷⁵ Sasa, Kanisa likitoka kwa Luther, Wesley, Pentekoste, itabidi lichongwe mpaka lile jiwe la Kichwani, Kristo Yesu, pamoja na Kanisa watakaa pamoja, haleluya, kulifunika Kanisa lote pamoja kwa ajili ya ufufuo wa kila mwanadamu aliyekufa akiamini Jina Lake. Amina. Ninaamini ya kwamba tupo hapa leo, ya kwamba Yesu Kristo angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini hilo?

¹⁷⁶ Kama angekuja katikati humu usiku huu, na angetenda na kufanya kama tu alivyofanya wakati huo . . .

¹⁷⁷ Unasema, “Je, Yeye angeniponya?”

Asingeweza kukuponya, tayari amekuponya.

“Je, Yeye angeniokoa?”

¹⁷⁸ Asingeweza kukuokoa, tayari amekuokoa, huna budi kulikubali. Angeweza kujionyesha Mwenyewe yupo hapa, angeweza kukuthibitishia kwa mtakatifu fulani *huko* nyuma kunena kwa lugha, na *huyu* kufasiri, ama njia nyingine kama hiyo, ama na—nabii ainuke na kusema jambo fulani lilikuwa ni kweli kabisa, ama kufanya jambo ambalo Maandiko yalisema ya kwamba angefanya katika siku za mwisho, ndipo ungeweza kuamini Yeye alikuwa akiishi pamoja nasi, Yeye alikuwa ndani yetu.

¹⁷⁹ Paulo alisema, “Ninyi nyote mkinena kwa lugha, wala hakuna mwenye kufasiri, mjinga aketi katikati,” kasema, “basi si wataondoka na kusema ninyi ni wendawazimu au mna kichaa?” Mnaona? “Lakini kama mtu ni nabii na anatabiri na kuzifunua siri za moyo, basi wote wataanguka chini, waseme, ‘Mungu yu pamoja nanyi.’”

180 Hiyo ni kweli? Vema, sote tunajua hiyo ni kweli. Basi kama walikuwa na hilo katika Kanisa la mwanzoni, hatuna budi kuwa nalo katika Kanisa hili mwishoni mwa wakati huu wa Mataifa; tuko katika wakati wa mwisho. Nami ninaamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

181 Nawe unasema, “Bwana, ningependa kumwona Yesu.”

182 Ninatumaini usiku wa leo kwa moyo wangu wote ya kwamba atajitambulisha miongoni mweni. Sasa, Yeye atafanyaje hilo? Vile vile alivyofanya wakati huo, vivyo hivyo tu alivyofanya wakati huo. Yeye aliahidi jambo hilo, alisema itakuwa katika siku za mwisho, tunaamini hizi ni siku za mwisho, ishara za siku za mwisho zinaonekana kila mahali, kanisa linapoa, mambo yote yakiendelea jinsi yanavyoendelea, kungekuwa na ukengeufu, mambo yote yaliyonenwa, lakini katika siku hiyo, Yeye aliahidi mambo haya yangetukia, nayo haya hapa.

183 Hivi mliona wakati Yesu alipoanza huduma Yake, jinsi alivyoanza, si kusema mengi sana kuhusu siku Zake wakati huo, alikuwa akisema mengi zaidi juu ya Kuja Kwake mara ya Pili kuliko alivyokuwa akisema juu ya kuja Kwake mara ya kwanza duniani? Akinena vile hili lingekuwa katika siku hii.

184 Sasa, kama atakuja . . . Sasa, haidhuru angekuwa na karama ya namna gani akisimama hapa, ama karama huko nje, hawana budi kukusanyika pamoja, huna budi kuamini la sivyo hakuna kitakachotukia. Maskini yule mwanamke aligusa vazi Lake naye akaponywa, kwa sababu aliliamini, alikuwa na imani. Mwanamke huyo alijipenyeza kwenye umati, labda yeye, tuseme walikuwa na kadi za maombi wakati huo, hawakuwa nazo, lakini tuseme walikuwa nazo, asingeweza kumfikia, hakuwa na njia ya kumfikia, hakuwa na njia ya kumfikia.

185 Kuna watu huko nje kwenye kusanyiko usiku wa leo, hawatakuwa na njia ya kufika hapa juu kuombewa, hatuna budi kuwachukua kama tu nambari yao inavyokuja. Vema, hiyo ni . . . Tutamchukua kila mtu tuwezaye, na kabla . . . Kila mwanamume aliye na kadi ya maombi, mwanamke, ishikilie tu, tutakufikia hapana shaka, hatujui jinsi itakavyokuwa, bali ni jinsi Roho atakavyoiongoza.

186 Sasa, maskini mwanamke huyu, alifanya nini? Alisema, “Kama nitagusa tu vazi Lake, ninaamini Mtu huyo alisema kweli, nitaninii, ni—ninajua nitaponywa.”

187 Mbona, bila shaka, hivyo ndivyo alivyoahidi. Vema. Imani yake . . . Ndipo basi wakati alipomgusa, loo, kila mtu alikuwa akimgusa, jamani, huku wakimkumbatia, na, “Hosana!” na wengine wakipiga mayowe, wakikosoa, na kila kitu. Bila shaka huo ni umati uliochanganyikana tena, umati, Makusanyiko ya Kristo sikuzote humzaa mwaminio, asiyeamini, na anayejifanya mwaminio.

¹⁸⁸ Sasa, walipokuja, ndipo akaligusa vazi Lake, naye akaondoka kwenye hilo kusanyiko, kama mlivyo usiku wa leo, na kuketi chini, labda. Labda alisimama, sijui. Hata hivyo, Yesu aligeuka, akasema, “Ni nani aliyenigusa?”

Kiasi kwamba, hata mtume Petro akamkemea, na kusema, “Kwa nini unasema jambo kama hilo? Kila mtu anakugusa Wewe.”

¹⁸⁹ Akasema, “Lakini naona kwamba nguvu zimenitoka.” *Nguvu* ni uweza, Yeye akawa dhaifu. Akamgusa, akadhoofika, akaangalia kwenye kusanyiko, mpaka akamwona, na kumwambia kuhusu kutokwa kwake na damu. Na tangu dakika iyo hiyo, aliamini ya kwamba ameponywa, naye aliponywa. Hiyo ni kweli?

¹⁹⁰ Sasa, kama Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, mnaamini ya kwamba Yeye ni...? Agano Jipya, Kitabu cha Waebrania kinasema ya kwamba Yeye, sasa hivi, ameketi mkono wa kuume wa Mungu, mamlaka huko Juu, Naye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli, ndugu? Sasa, kama umeketi huko nje wala si kwenye mstari wa maombi hapa, kama unaamini kwa moyo wako wote, wewe ni mgonjwa, sema, “Bwana Mungu, mimi ni mgonjwa, pia, ninahitaji usaidizi. Utanisaidia, Ee Bwana?” Uone yale afanyayo. Bila shaka.

¹⁹¹ Kama utamwamini kwa moyo wako wote, Yeye ni Kuhani Mkuu... Haingefaa chochote kunigusa mimi, mimi ni mwenye dhambi tu aliyeokolewa kwa neema. Haitafaa chochote kumgusa yeyote katika sisi wengine, sisi ni wenye dhambi tu waliookolewa kwa neema. Lakini kama utaiacha roho yako itupite, na kwenda huko juu, na kusema, “Bwana Mungu, ninaamini kwa moyo wako wote ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Hizi ndizo ishara ulizosema, mtu huyo alilisoma kutoka katika Biblia, ama, alilisema kutoka katika Biblia. Nitaisoma, nimeisoma mara nyingi, ninaijua, na ninaamini ya kwamba ni kweli.”

¹⁹² Wakati... Kama atakuja miongoni mwetu usiku wa leo, Sisemi kwamba atakuja, lakini kama atakuja, basi sema, “Nijalie, Ee Bwana Mungu.” Ndipo uguse vazi Lake, uone kama Yeye hatageuka moja kwa moja, afanye jambo lile lile alilofanya jana. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.

Na tuombe.

¹⁹³ Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha sana kuwa watumishi Wako. Tuna furaha sana kujua ya kwamba Wewe u hai, na—na katika siku hii kuu ambapo tunajulikana kwa mzunguko wa historia, tunajua kwa mujibu wa mwonekano wa mambo, tunajua kwa jinsi UN na mataifa mbalimbali yanavyoendelea hatuko hapa muda mrefu zaidi, tunajua ya kwamba hivi karibuni mtu fulani atafanya kosa fulani, watarusha moja ya makombora hayo.

¹⁹⁴ Na kote ulimwenguni, visiwa vikubwa vilivyojaa makombora ya atomiki, mabomu ya haidrojeni ambayo yataenea maili mia moja na sabini na tano mraba, kina cha futi mia moja na hamsini ardhini, na maelfu ya hayo yanalenga kila mji kote katika taifa hili, na kote ulimwenguni, kutoka upande mmoja hadi mwingine. Na mara ya kwanza moja la hayo litakapoingia kwenye skri—skrini, huyo mwingine ataachilia, ulimwengu usingeweza kustahimili jambo hilo, Bwana, na kabla haya yote hayajatukia, Wewe ulisema tutaondoka. Kule Kuja kumekaribia jinsi gani basi? Kama tungeweza kutazamia hilo saa yoyote, ni zaidi sana vipi kule Kuja kwa Bwana?

¹⁹⁵ Sasa, Baba Mungu, tunajua ya kwamba ni kundi dogo tu letu hapa usiku wa leo, bali tuko hapa na... tukitumaini, Bwana, kwamba tuko katika nia moja, tunaamini. Na hili ambalo tumeshikilia... Hawa hapa wahudumu wameketi jukwaani, muda mrefu kabla sijaanza kuhubiri, walikuwa ni wahudumu wakihubiri Injili. Kuna wengi huko nje vivyo hivyo, walionena na kutabiri juu ya siku hii. Tunakaribia mwisho, Baba. Muda ni mfupi sana, tunajaribu kushindilia mengi sana usiku mmoja. Tunafikiri labda huenda kukawa na mwenye dhambi hapa ambaye asingekuwa hapa tena kesho usiku, ishike nafsi yake usiku wa leo, Bwana. Tujalie.

¹⁹⁶ Sasa, jalia Roho Mtakatifu aje usiku wa leo. Atutie mafuta, alitie kusanyiko mafuta, awatie mafuta hawa wahudumu jukwaani, anitie mimi mafuta, mtumishi Wako asiyestahili. Naomba ututumie, Bwana, kulitimiza Neno Lako uliloahidi ya kwamba ungetimiza, ulisema, "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona tena." Hiyo ni kweli, Bwana.

¹⁹⁷ Mkutano huu ulitangazwa juu, chini mitaani, kila mahali. Ulimwengu ungali ukijishughulikia, maji yanapenya kiwango chake, lakini kuna wengine ambao wamejipenyeza kwenye joto, wakaketi katika jengo hili dogo usiku wa leo, wanaona njaa, wanaona kiu, wanakupenda, wanataka kujua zaidi kukuhusu Wewe. Nami nimesimama hapa kwa Neno Lako, nikiwaambia ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele kuwatia moyo. Kama wana njaa kwa ajili Yako, Wewe upo hapa kuwaokoa; kama wana njaa kwa ajili ya uponyaji, Wewe upo hapa kuwaponya. Uwepo Wako wenyewe upo hapa, Nao utawaponya kama wataamini; utawaokoa kama wataamini.

¹⁹⁸ Kwa hiyo, Baba Mungu, njoo usiku wa leo na ufanye jambo kama ulivyofanya huko nyuma. Na hilo lilikuwa thibitisho kwa wale waliokuwa wakitoka Emau kama tulivyotaja muda mfupi uliopita, wao, ilikuwa ni thibitisho kwao ya kwamba Wewe ulikuwa ni Yesu aliyefufuka, si mwingine, Yeye yule, kwa kuwa Wewe ulifanya mambo yale yale uliyofanya kabla ya kusulubiwa Kwako, walijua Wewe ulikuwa hai.

¹⁹⁹ Baba Mungu, huenda kukawa na wanaume na wanawake hapa ndani usiku wa leo ambao hawajapitia jambo hili bado, jalia walipitie usiku wa leo, ni kwa ajili ya heshima Yako, Bwana, na utukufu Wako. Ninajikabidhi mwenyewe kwako, pamoja na kanisa lote, kwamba utatutumia kwa heshima Yako. Katika Jina la Yesu, ninaomba. Amina.

²⁰⁰ Kama kungekuwa na njia kwangu ya kuwaponya wagonjwa, bila shaka ningefanya hivyo, ningefurahi kufanya hivyo. Sina nguvu za kuponya, siamini mtu mwingine yeyote anazo. Wanaume... Siamini daktari anazo, ninaamini uponyaji unakaa katika Mungu. Daktari ana haki, anaweza kutoa kitu fulani, ama kung'oa jino, kushona kitu fulani, kutoa kidole tumbo, ama jipu, ama chochote kile, bali yeye hajengi tishu, wala dawa haijengi, maumbile, Mungu hufanya hilo, hiyo ni kweli, yote kutoka kwa Mungu. Ukivunjika mkono wako, unaenda kwa daktari na kumwacha aurudishe, lakini hauponyi, anaurudisha tu, Mungu huponya, Yeye anauponya, hutoa kalisi na chochote kinachoingia kwenye mifupa ku—kuuponya.

²⁰¹ Sasa, ni wangapi hapa ndani walio wagonjwa usiku wa leo? Inua mkono wako, ambaye ni mgonjwa na unahitaji uponyaji mwilini mwako, nusu ya kusanyiko. Sasa, mwanangu aligawa kadi za maombi, hatuna nafasi ya kuwaita wote kwa wakati mmoja. Lakini hebu tuwaite tu wachache, kisha baadaye, tutawachukua waliosalia, labda usiku wa leo, labda sivyo, kesho usiku, ama usiku unaofuata, ama wakati wowote Bwana anapotenda kazi.

²⁰² Lakini sasa kumbukeni, ninasema hivi: sisemi kwamba atafanya hivyo. Sasa, mimi... Hiyo ni juu Yake, sina njia ya kuhakikisha kwamba itafanyika, Lakini Yeye hajanipungukia bado, mbele ya kadiri ya laki tano kwa wakati mmoja, na Yeye—Yeye hatanipungukia usiku wa leo, nami nina hakika hatanipungukia.

²⁰³ Sasa, hebu na tuache kadi za maombi... Sasa, kadi ya maombi ina namba juu yake, nazo ni namba moja, mbili, tatu, nne, tano, namna hiyo. Hatuwezi kuwasimamisha wote. Ama nadhani alianza kwenye moja, nadhani moja. Yuko wapi? Kuna mtu aliye na kadi ya maombi, namba moja? Inua mkono wako, hebu tuone. Huyu mvulana hayupo hapa. Kuna kadi ya maombi, namba moja? Mtu ana kadi ya maombi, moja? Vema, labda nina... Labda hazikuanzia... Ama huyu—huyu mama mweusi hapa? Vema. Njoo papa hapa, mama, moja kwa moja upande huu.

²⁰⁴ Kadi ya maombi namba mbili, waweza kuinua mkono wako, yeyote aliye nayo? Huyu muungwana? Papa hapa, bwana. Kadi ya maombi namba tatu. Vema, mama, njoo papa hapa. Namba nne, nne. Vema. Namba tano. Ni nani aliye na kadi ya maombi namba tano? Waweza kuinua mkono wako, yeyote aliye nayo? Je, mama huyu hapa ana...? Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita.

205 Sababu ya mimi kuwaita mmoja mmoja, maana mtu fulani huenda akawa ni kiziwi wala hawezi kusikia. Namba sita. Njoo huku. Kama huwezi kusimama, tuna...Hawa ni mabawabu walosimama hapa? Loo, sawa. Wa—watakubeba kama huwezi kuja. Vema. Namba sita, saba. Waweza tu kuinua mkono wako, upesi tafadhali? Angalia kadi yako ya maombi. Namba saba. Vema. Nane, nane. Kadi ya maombi nane. Labda wao... .

206 Sasa, kama ukipata kadi ya maombi, iweke mwenyewe, usiichukue na kumpa jirani, acha jirani aje asikie maagizo, pia, kama wataombewa. Kadi za maombi hazibadilishanwi, utaondolewa mstarini. Unaona? Sasa, lazima uisikie huo ujumbe mwenyewe, uje mwenyewe. Na sasa, kama ukikosa zamu yako, basi kumbuka tuliita namba yako. Nane haipo? Usichukue moja kisha uondoke jengoni. Kaa nayo, kaa hapa.

207 Vema, nane, tisa, tisa. Mtu aliye na kadi ya maombi...? Vema, mlete huyo mama. Kumi, kumi na moja. Hiyo ni kweli. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na mbili. Hakuna kumi na mbili, kumi na moja au kumi na mbili? Kumi na tatu, kumi na tatu. Hakuna kumi na tatu? Kumi na nne, kumi na nne, kumi na tatu. Je, mama huyo ana kumi na tatu? Vema. Wasemaje? Vema. Kumi na tatu, kumi na nne, kumi na nne, kumi na tano.

208 Sababu ya sisi kuwaita, si uwanja wa michezo, ni—ni kanisa, mwajua, ambapo... U—umekuwa mikutanoni na kuona wakati wao, loo, wanakanyagana tu wao kwa wao, na loo, ni kukosa kicho kabisa. Kwa hiyo hatutaki... Tunataka uchaji na heshima kwa Injili.

209 Kumi na tano, je, mtu huyo alikuja? Kumi na tano, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa. Vema, ni—ni hizo tu? Vema, hiyo ni... Uligawa ngapi? Hamsini na kitu. Vema, sawa. Labda wengine, unakuwa na aibu kidogo na kurudi nyuma. Hebu wasimame pale. Vema.

210 Hebu, kila mtu awe na kicho sasa, sasa mtu yeyote asisogee huku na huku, iweni na kicho. Ni wangapi waliopata kuona ile picha ambayo sayansi imepiga ya yule Malaika wa Bwana, moja kwa moja jengoni? Leo, unazo, mwanangu? Leo? Wameichukua. Ni, Washington, DC, ina hakimiliki, Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichopata kupigwa picha, Nguzo ile ile ya Moto iliyowaongoza wana wa Israeli. Kulikuwa na moja iliyopigwa papa hapa California hivi majuzi tu, wakati Yeye alipokuwa pale jukwaani. Sasa, Yeye... Hiyo ni... Yeye ni ninii tu... Yeye... .

211 Yesu alisema, “Nilitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu.” Ni wangapi wanajua Yeye alisema hivyo? Alitoka kwa Mungu. Yesu alikuwa—alikuwa nini wakati alipokuja kwa wana wa Israeli? Alikuwa ni Malaika wa agano, tunajua hilo. Vema, Yeye alikuwa Ngu—Nguzo ya Moto iliyokuwa katika kichaka kilichowaka moto. Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaoamini hilo?

Semeni, “Amina.” Vema. Ndipo wakati alipokufa, akafufuka tena, kisha akarudi kwa Baba, halafu alipokutana na Paulo akienda zake Dameski, Yeye alikuwa ni nini? Nguzo ile ile ya Moto, Nuru iliyoyapofusha macho ya Paulo. Uh-huh. Mnaona? “Nilitoka kwa Mungu, ninaenda kwa Mungu.”

²¹² Na Yesu yuyo huyo ameonekana hata kwa jicho la kimitambo. Wakati George J. Lacy, mkuu wa FBI, wa alama za vidole na hati, alipoichunguza picha hiyo, alisema, “Nuru iligusa lenzi.” Akaweka ushuhuda, akauandika, akatia sahihi jina lake kwake.

²¹³ Lakini basi a—akasema, “Bw. Branham, wakati mmoja mimi mwenyewe nilikukosoa.” Kasema, “Nilisema ilikuwa ni saikolojia.” Akasema, “Lakini ninii... Nilisema ulikuwa ukisoma mawazo ya hao watu.” Akasema, “Lakini jicho la kimitambo la kamera hii halipigi picha saikolojia, Nuru iligusa lenzi.”

²¹⁴ Hiyo hapo, picha kubwa iliyopigwa; waliipiga mara nne ama tano zaidi. Waliipiga Ujerumani hapa si muda mrefu uliopita, picha tatu mbalimbali, ikishuka, wakati ilipokuwa inatia mafuta, ikiondoka. Ujerumani ilisema jambo lile lile chini ya uchunguzi wao. Ujerumani, Uswisi. Mnaona hapo? Si...

²¹⁵ Enyi marafiki, hatuigizi kanisa, tunaishi katika Uwepo wa Bwana Yesu. Sasa, ninawatakeni mkumbuke hilo. Sasa, huu mkutano ni mkutano wenu.

²¹⁶ Sasa, ni watu wangapi huko nje ambao hatufahamiani, siwajui? Inueni mikono yenu. Unajua ya kwamba sikujui, au sijui lolote kukuhusu, inueni mikono yenu. Unajua wewe ni mgonjwa... naam. Vema, nadhani kusanyiko lote. Kadiri ninavyoweza kuona, hakuna mtu hapa ninayemjua. Mwanangu mwenyewe, Ndugu Borders, nilikutana na ndugu mhudumu pale, nafikiri nimemwona hapo awali, lakini si—siwezi kabisa kumweka, nimekuwa nikijaribu akilini mwangu, nje ya hao, simjui mtu yeyote.

²¹⁷ Ni wangapi katika mstari wa maombi wanaojua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, wala lolote kuhusu...? Inueni mikono yenu, ninyi mlio kwenye mstari wa maombi, mimi ni mgeni kwenu. Hii *hapa* mikono yangu, sijui hata mmoja wao, na hii *hapa* Biblia yangu.

²¹⁸ Sasa, watu hao, labda wao ni wagonjwa, labda si wagonjwa, sijui, huenda wakawa na shida za kifedha, huenda... Sijui ni nini, mambo ya nyumbani, sijui, bali Bwana Yesu anajua. Hiyo ni kweli?

²¹⁹ Ni wangapi wenu walio huko nje ambao hawana kadi ya maombi, nanyi ni wagonjwa, na mnataka Yesu awaponye? Inua mkono wako. Kila mahali, pia? Vema, nadhani ni kila mahali. Mnaona? Vema. Iweni tu na imani, aminini kwa moyo wenu wote sasa, iweni tu na imani. Na wakati... Kama Bwana akija na

kuanza kuwabariki watu, basi useme, “Bwana, nijalie, pia.” Basi angalia uone kama Yeye hakufanyii jambo lile lile analofanya jukwaani. Hii ni kuwaleta tu baadhi ya watu hapa juu, kusudi mpate kuona, si kitu ila papa hapa jukwaani ambapo kila mtu anaangalia.

²²⁰ Sasa, mama huyu hapa... Sasa, kama atafanya vile vile usiku wa leo alivyofanya katika siku zilizopita, ni wangapi wataamini ya kwamba Yeye yupo hapa? Inua mkono wako. Loo, asanteni. Hiyo ni... Ukiendelea na hilo, utaona mkutano mkubwa hapa katika—katika siku kumi zijazo, endeeleni na imani hiyo. Hiyo ndiyo... Mara tu mlipofanya hivyo, kitu fulani kilinyanyuliwa kutoka kwangu, mnaona, upako ulishuka juu yangu papo hapo. Um-hum. Sasa Yeye yupo hapa, sasa hivi, Uwepo wa Bwana.

²²¹ Nina furaha sana kujua, usiku wa leo, ya kwamba—ya kwamba wewe—wewe ukiwa ni dada mweusi aliyesimama hapa. Sasa, hili linanirudisha kwenye yale niliyozungumzia. Katika Yohana Mtakatifu mlango wa 4 kulikuwako na Mwanamume na mwanamke waliokutana, ambao walikuwa ni Myahudi na Msamaria, jamii mbili za watu, mara ya kwanza waliyowahi kukutana maishani mwao. Hiyo ni kweli? Unaamini hilo? Inua mikono yako, endapo wewe... Hiyo ni kweli, mara ya kwanza walipopata kukutana.

²²² Ndipo Yesu akamwambia yule mwanamke, akamwomba maji anywe. Akaanza kuzungumza naye. Mnafikiri alifanya hivyo kwa sababu gani? Ilikuwa ni kusudi awasiliane na roho yake. Mnaona? Kuwasiliana. Baba... Alisema alikuwa na haja ya kupitia, Baba alimtuma huko, kama alivyofanya, kama ungefungua mlango unaofuata, ambapo tutafikia labda kesho usiku, yule mtu kisimani, uh, mtu chini ya yale matao matano, mfano mzuri pale, jinsi alivyomjia mtu huyo mmoja, akampita kilema, kiwete, kipofu, aliyepooza, akaenda kwa mtu huyo mmoja, kwa kuwa Yeye alijua ya kwamba alikuwa hivi. Mnaona, Baba alikuwa amentuma.

²²³ Ndipo akageuka na kusema, Yohana Mtakatifu 5:19, walimwuliza kwa nini hakuwaponya wote, ama kadhalika, wakamhukumu mtu huyu kwa kubeba kitanda chake siku ya Sabato, akasema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda.” Hiyo ni kweli? Ndipo Yesu hakufanya jambo moja mpaka Yeye... Mungu alipomwonyesha ono afanye nini. Je, hayo ni Maandiko?

²²⁴ Sikilizeni, hebu nilinukuu, Yohana Mtakatifu 5:19, “Amin, amin,” hiyo ni *kabisa, kabisa*, “nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona,” si analosikia, “lile ambalo amwona Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile. Baba anatenda kazi, Nami natenda kazi hata sasa.”

225 Hilo, kwa maneno mengine, Yeye alisema, “Sitendi neno mpaka nitakapomwona Baba akinionyesha ono, kwanza, kwamba nitende nini, kisha ninalitenda.”

226 Hivi majuzi usiku nilipokutana na Dk. Lamsa, wa Biblia ya Lamsa, alisema, “Watu hawa wa Marekani wana shida gani?”

227 Kasema, “Sijui. Asilimia sabini ya Biblia ni ono, hata hivyo hawawezi kuamini.” Mnaona?

228 Hii ni kama tu ilivyokuwa huko Samaria, jamii mbili za watu, mimi ni Mwairishi, yeye ni Mwafrika. Tunakutana hapa kwa mara ya kwanza katika mandhari ndogo, wawili walikutana. Katika siku hizo kulikuwako na ubaguzi, Yesu alimjulisha upesi sana hakuna tofauti kati ya rangi ya mtu mbele za Mungu. Sisi sote tunatoka katika familia moja: Adamu na Hawa. Nchi tulimoishi na ikabadilisha rangi zetu, manjano, hudhurungi, nyeusi, nyeupe, haina uhusiano wowote na Mungu, tunaweza kupeana damu. Damu moja, Mungu aliwaumba watu wote. Mnaamini hilo? Naam, bwana. Hawa . . .

229 Ambapo mmoja aliishi katika nchi yenye joto na mwingine nchi yenye baridi, na—na namna hiyo, wenye hasira, na kadhalika, ilibadilisha rangi zao, hilo halina uhusiano wowote na damu, wala nafsi, wala chochote kile. Mungu alimfanya ajue ya kwamba Mungu anawatafuta wale watakaomwabudu katika roho na kweli.

230 Sasa, mwanamke huyu, hatufahamiani. Sasa, sijawahi kumwona maishani mwangu, labda hajawahi kuniona maishani mwake, nasi hapa tunakutana kwa mara ya kwanza, kama yule mwanamke kisimani na Bwana wetu. Sasa, kama Bwana wetu angali yeye yule, na kama Yeye ataninii . . .

231 Sasa, kama huyo mwanamke ni mgonjwa, nami ningeweza kusema, “Vema, mama, wewe ni mgonjwa, njoo hapa juu.” Apande juu, nimwekee mikono, niseme, “Namtoa huyu pepo mchafu,” ama nipige miguu yangu chini, ama chochote kile, niseme, “Shetani, toka ndani yake. Nenda nyumbani, mama, upate afya.” Hilo lingeweza kuwa sawa, hilo ni la Kimaandiko. Bila shaka. “Kwa Jina Langu watatoa pepo.”

232 Ndugu wengi wana huduma kama hizo, zilizofanikiwa zaidi sana kuliko yangu, Oral Roberts, kwa mfano, mnaona. Huduma yangu haikolei Marekani, inakolea nchi za ng’ambo, basi, inafanikiwa sana basi. Niliwaona makafiri elfu thelathini wakimjia Kristo katika wito mmoja wa madhabahuni, jambo fulani lilitukia jukwaani, nikimwambia tu mmoja, kuona mwujiza ukifanywa, wenyeji thelathini elfu wanaovaa blanketi walivunjilia sanamu zao ardhini, wakamjia Kristo, Durban, Afrika Kusini.

233 Sasa, kama hatufahamiani, Bwana Yesu anamjua na Yeye ananijua mimi. Sasa, kama Yeye atamwambia jambo fulani ambalo amefanya, ama jambo fulani analokusudia kufanya, ama

jambo fulani ambalo anajua kwamba sijui chochote kulihusu, basi hakika, kama Yeye anaweza kumwambia kile ambacho amekuwa, bila shaka anaweza kujua atakavyokuwa. Hiyo ni kweli? Sasa, hilo lingekuwa kubwa zaidi jinsi gani kama Kitu fulani kingemwambia, kama jambo fulani lililotukia katika Biblia, na kingemwambia hivyo? Je, kama angefanya hivyo, ungeamini Yeye alikuwa ni Bwana yeye yule? Ungeamini.

²³⁴ Unajua isingekuwa ni ndugu yenu hapa, inanibidi tu kuisalimisha roho yangu. Mimi ni kama tu maikrofoni hii, bubu mpaka Yeye atakaponena, maana ni mtu gani angejua hilo? Hakuna. Inahitaji Mungu kufanya hivyo. Sasa, kama Mungu atanijulisha kwa kuzungumza tu nawe... Naam, bwana, ninajaribu kuwasiliana na roho yako. Hiyo ni kweli kabisa. Sasa ndio kwanza itoke upesi kwa wasikilizaji, na hiyo ni kweli.

²³⁵ Sasa, kama Yeye ataniambia jambo fulani kukuhusu wewe, jambo fulani lililokuleta hapa, kama yule mwanamke kisimani, ama kama yule mwanamke aliyekuwa anatokwa damu, ama kitu fulani, basi uta—uta—utaamini kwa moyo wako wote. Ni wangapi huko nje watakaoamini, pia, wakati hapa, mimi na mwanamke huyu hapa, hatufahamiani, sijawahi kumwona maishani mwangu mpaka sasa hivi?

²³⁶ Sasa, na afanye hivyo, ninatumaini ya kwamba atafanya. Na kama akifanya hivyo, basi itakupa imani, ikufanye ujisikie umehakikishiwa kwamba Yeye anakupenda, na Yeye anajua habari zako. Na kama Yeye anajua habari zako, Yeye anajua habari za kila mtu huko nje, kwa hiyo basi hiyo inaonyesha tu Yeye Yupo. Kwa hiyo hilo lingemfanya tu kila mtu kumkubali, na apate kuwa mzima. Hiyo ni kweli? Ama wamkubali Yeye kama Mwokozi wao, na waokolewe.

²³⁷ Sasa, kama mtu yeyote bado anaweza kunisikia: ninakuja kuchukua kila roho humu ndani katika Jina la Yesu Kristo. Na mwanamke huyu, ambaye anajua sasa kwamba jambo fulani linaendelea, huyu mama anaugua ugonjwa mbaya sana wa wasiwasi. Hiyo ni kweli. Ni kweli tu, wasiwasi kabisa. Hiyo ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sasa unaamini?

²³⁸ Sasa, ilikuwa ni nini, sijui nilichosema, lakini ilimwambia jambo fulani. Nilimwona akifanya jambo fulani, akionekana kana kwamba alikuwa akijaribu kukunja mikono yake, ama kitu fulani, ama kufadhaikia jambo fulani, *jambo lingine*.

Unasema, “Ndugu Branham, ulibahatisha hilo.”

²³⁹ Sikulibahatisha. Lingewezaje kuwa kamilifu kila wakati kati ya makumi ya maelfu, mara maelfu? Kama unafikiri nilibahatisha, hebu nizungumze na mwanamke huyo kwa muda mrefu kidogo. Ni mkutano wenu.

²⁴⁰ Mnaona, alionekana kama mtu mzuri kwangu. Mimi... Wewe ninii tu... Sitaki wewe... Acha tu akili yako itulie. U—unajua tu ya kwamba... Unaamini ya kwamba uko Mbele ya

Bwana Yesu? Sasa, unahisi hisia tamu sana. Hiyo si ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua tu mkono wako kwa watu. Unaona? Ninaangalia moja kwa moja kwenye Nuru inayoangazia papa hapa juu ya huyu mwanamke.

²⁴¹ Naam, amefadhaika kabisa, ana—ana wasiwasi, ana ugonjwa wa wasiwasi. Nawe una—unahusika ama unamwombea mtu mwingine. Kuna msichana mdogo, naye huyo msichana ana ugonjwa wa mafindofindo. Huyo ni yeye aliyeketi moja kwa moja huko nje. Hiyo ni kweli, sivyo? Vema, dada, imekwisha. Isitoshe, wewe ni mhudumu, wewe ni mwanamke mhubiri. Unaamini Mungu anajua wewe ni nani? Bibi Peters, haja yako imejibiwa. Wasiwasi wako umekwisha, nenda nyumbani ukapate afya, katika Jina la Bwana.

²⁴² Unaamini kwa moyo wako wote? Kuwa tu na imani, amini tu. Sasa, hivyo ndivyo alivyokuwa jana, hivyo ndivyo alivyo leo, ndivyo atakavyokuwa sikuzote. Sasa, kama alivyojidhihirisha Mwenyewe mbele ya Ibrahimu katika mwili wa kibinadamu, Yeye... Mungu alidhihirishwa katika Kristo. Mnaamini hilo? “Si Mimi nizitendaye hizo kazi, ni Baba Yangu anayekaa ndani Yangu.”

²⁴³ Sasa, hilo si lilikuwa rahisi, kuamini tu? Hata sikumwombea dua, bali aliponywa vivyo hivyo. Ni kitu gani kilichofanya hilo? Imani yake ilimponya, chochote kile. Vema.

²⁴⁴ U hali gani? Hatufahamiani, Bwana Yesu anatumia sote wawili. Sasa, sisi ni wanaume, umri tofauti, mara ya kwanza tumekutana. Kama Mungu atanifunulia shida yako ni nini, ama kitu fulani, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama mtumishi Wake, hasa? Utaamini hilo?

²⁴⁵ Unaugua sana ugonjwa wa tumbo, mbaya sana, sana. Hutoki kwenye mji huu, unatoka kwenye mji mwingine, uko huko nje katika nchi tambarare, ya ngano, unatoka Oklahoma, Tulsa, Oklahoma. Hiyo ni kweli. Wewe ni Mwitiliano kwa—kwa utaifa wako. Nawe ulikuwa kwenye mmoja wa mikutano yangu hapo awali, ilikuwa kwenye mkutano wa Tulsa, ukajaribu kuingia mstarini wala usingeweza kupata kadi ya maombi, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini kwa moyo wako wote sasa? Nenda, ukale chakula chako cha jioni, Yesu Kristo anakuponya. Nenda nyumbani ukashangilie. Mungu akubariki, bwana. Mungu awe pamoja nawe.

²⁴⁶ Unamwamini Bwana? Sasa, hata uwe nani, amini tu, usiwe na shaka. Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana. Unaamini hilo? Mambo yote yanawezekana kwao waaminio. Ni wangapi huko nje kwenye kusanyiko wana—wanaamini? Sema, “Ninaamini kwa moyo wangu wote.” Hakuna sababu ya wewe kutoponywa, amini tu.

²⁴⁷ U hali gani? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Hatufahamiani. Lakini unaamini ya kwamba Mungu anajua

yote kukuhusu? Unaamini ya kwamba Yeye anaweza kukupa afya na kukuponya? Vipi kama ningekwambia, uliponywa? Je, ungeniamini? Hakika ungeniamini.

²⁴⁸ Unataka mume wako aponywe, pia, sivyo? Unaamini ya kwamba Yeye atamponya? Unataka kujua shida yake...? Unataka nikwambie shida yake ni nini? Ugonjwa wa kibofu. Wewe una ugonjwa wa kike, daktari anasema mfuko wa uzazi unaodondoka, mfuko wa uzazi ulioanguka. Hiyo ni kweli. Wewe ni mhudumu, pia, wa Injili, mwanamke mhubiri. Nenda ukapokee uponyaji wako, Yesu Kristo anakuponya.

Amini, usiwe na shaka.

²⁴⁹ Unaamini kwa moyo wako wote, mama? Kama Mungu atanifunulia jambo fulani kukuhusu ambalo sijui... Hatufahamiani, sivyo? Kama atanifunulia jambo fulani ambalo unajua kwamba silijui, basi utajua Huyo si ndugu yako, ni Bwana wako. Hiyo ni kweli?

Mtu fulani mkutanoni, mahali fulani...

²⁵⁰ Unaugua ugonjwa ambao unapaswa kufanyiwa upasuaji, wanasema unapaswa kufanyiwa, ni kivimbe. Unaamini ninaweza kukwambia mahali hicho kivimbe kilipo kwa nguvu za Mungu? Ubavuni mwako, chini ya mkono wako wa kulia. Hiyo ni kweli. Nenda ukaamini kwa moyo wako wote, uponywe, katika Jina la Bwana Yesu.

Iweni tu na imani, msitilie shaka.

²⁵¹ U hali gani? Hatufahamiani, nadhani. Uliniona mara moja. Mkutanoni? Mkutanoni tu. Lakini ninamaanisha, sikujui, nawe hujui... Nikiwa nimeketi tu nje mkutanoni, uliniona mara moja. Vema, kama Bwana atanifunulia siri ya moyo wako, aniambie jambo fulani ambalo umefanya, ama unalopanga kufanya, ama shida uliyo nayo, ama—ama *kitu fulani*, wewe, basi utajua haina budi kuwa ni Mungu, haina budi kuwa ni Roho, isingeweza kuwa ni mimi.

²⁵² Ugonjwa wa tumbo, ugonjwa wa koo, halafu una mzigo moyoni mwako. Ni mvulana. Niseme? Yuko kwenye nyumba ya watoto, ana ugonjwa wa moyo. Mwamini Bwana Yesu, na Mungu atamwokoa na jambo hili.

Amini. Unaamini kwa moyo wako wote?

²⁵³ Sasa, ili mpate kujua si telepathia: Mama huyu hapa, njoo hapa, mama, simjui huyu mama. Weka tu mkono wako juu ya wangu. Kama Bwana Yesu atanionyesha hivi shida yako, utaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Unaamini? Vema, basi ugonjwa wako wa moyo unakuacha. Mwamini Mungu, amini kwa moyo wako wote.

²⁵⁴ Sasa, nilipomwambia hivyo, ulipata hisia ya ajabu sana nilipomwambia hivyo, kwa sababu ulikuwa na ugonjwa wa moyo, pia. Nenda ukiamini kwa moyo wako wote, na upate afya.

Mnaamini kwa mioyo yenu yote? Vema.

255 Sasa, mama huyu hana budi kuponywa la sivyo afe. Je, unajua shida yako? Umetiwa uvuli wa mauti, kansa. Lakini unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuiondoa kansa hiyo? Njoo hapa.

256 Shetani, ninakuamuru kwa Damu ya Yesu Kristo, mateso Yake ya uwakilishi pale Kalvari, ushindi Wake juu yako, na wote walio kama wewe, katika Jina la Yesu Kristo, toka ndani ya mwanamke huyu na umwache! Amina.

Nenda, ukiamini kwa moyo wako wote.

Wasiwasi, ugonjwa wa moyo, nenda ukaamini, upate afya, katika Jina la Bwana Yesu.

257 Njoo, mama. Unazungumza Kiingereza? Kama Bwana atanifunulia shida yako ni nini, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya basi? Unaamini? Vema. Ni shida ya wanawake, shida ya kike. Nenda ukaamini, na Bwana Yesu atakomesha hayo yote...?...na kadhalika.

258 "Kama unaweza kuamini!"

259 Unaamini Mungu atakuponya ugonjwa huo wa moyo, akupe afya? Unaamini? Je, utaachana na kitu fulani kwa ajili Yake? Unataka kuziacha, kwa vyovyote vile: sigara. Zitupilie mbali, usivute sigara tena.

260 Kumbukeni, msije hapa na dhambi, Yeye anaijua, mnaona.

261 Vema, njoo ukiamini kwa moyo wako wote. Vema, njoo. Mlete, dada. Hilo ni sawa. Kama nikiweka mikono juu yako, unaamini utapona?

Bwana Yesu, tujalie, naomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Amini sasa kwa moyo wako wote, uone kama hutapata afya. Sasa aminini.

Wasiwasi si kitu kwa Mungu. Unaamini Yeye atakuponya? Nenda, ukiamini basi, na Bwana Yesu akuponye na kufanya...

262 Huyo mama aliyeketi hapo karibu na huyo anayepaza sauti, ana shida fulani na mkono wake, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya ukiketi hapo, mama? Sasa, ulimgusa Nani? Ulimgusa Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wako, alikuponya. Nenda nyumbani, na uamini kwa moyo wako wote.

263 Niambieni aligusa nini. Kamwe hakunigusa mimi, yeye yuko mbali sana nami. Mnaamini kwa mioyo yenu yote sasa?

264 Mama aliyeketi huko nyuma, akilia mwishoni, akiwa na ugonjwa huo wa kibofu, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, mama? Vema. Leso mpaka kinywani mwako, ukilia, namna *hii*, vema? Unaamini kwa moyo wako wote? Unaugua ugonjwa wa kibofu, kinachoma sana, na kwa hiyo... Unaamini

kwa moyo wako wote sasa? Simama kwa miguu yako na ukubali uponyaji wako.

²⁶⁵ Ninamwamuru huyo pepo, katika Jina la Yesu Kristo, amwache huyo mwaminio!

²⁶⁶ Mwaminini Mungu, msitilie shaka. Mwaminini Mungu.

²⁶⁷ Mtu aliyeketi moja kwa moja huko nyuma akiugua bawasiri, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, bwana? Simama kwa miguu yako, ukubali ninii yako... Uligusa nini? Uko yadi ishirini kutoka kwangu. Ulimgusa Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Nenda nyumbani ukapate afya. Yesu Kristo akuponye.

Unaweza kuamini? Kila mtu anaweza kuamini?

Na wewe je? Huyu, huyo mama, loo, ninamjua mwanamke huyo, huyo ni Dada Dauch aliyeketi hapo, ninamjua.

²⁶⁸ Mwanamume huyo karibu naye, ulikuwa umeinua mkono wako, sivyo, bwana? Unaamini kwa moyo wako wote? Nilimwona Malaika wa Bwana akitokea hapo. Unaamini huo ugonjwa wa mgongo utakuacha? Vema. Hiyo ndiyo iliyokuwa shida yako, sivyo? Tikisa mkono wako namna *hii*, kama hiyo ni kweli. Punga mkono wako mbele na nyuma. Vema, nenda nyumbani, unapokea uponyaji wako. Yesu Kristo anakuponya.

Geuka urudi nje ya jukwaa pale, bwana. Ugonjwa wa moyo ulikuacha, nawe unaweza kwenda nyumbani, ukaponywe sasa. Mungu akubariki.

²⁶⁹ Unamwamini Bwana Yesu Kristo? Ni wangapi hapa ambao si Mkristo, ambaye si Mkristo, unayetaka kumkubali Bwana kama Mwokozi wako binafsi? Simama kwa miguu yako sasa hivi, wakati ukiwa katika Uwepo Wake. Mtu fulani ambaye amerudi nyuma, anataka kumjia Bwana, uko moja kwa moja katika Uwepo Wake. Unamwamini? Simama kwa miguu yako sasa hivi, tutakuombea. Kama utasimama kwa miguu yako, mwenye dhambi yeyote, yeyote aliyerudi nyuma. Mungu akubariki. Mtu mwingine?

²⁷⁰ Bwana, ninalaani uovu ambao umekusumbua miaka hii yote. Katika Jina la Yesu Kristo, umesamehewa dhambi zako. Nenda, amini kwa moyo wako wote.

Mtu mwingine angesimama, na kusema, “Ninataka kumkubali Yesu”?

²⁷¹ Ni wangapi wenu hapa walio wagonjwa, na mnaamini ya kwamba Yeye yupo hapa katika Uwepo Wake, katika nguvu Zake? Inua mkono wako. Ni wangapi wanaojua Biblia ilisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio”? Wangapi wenu ni waaminio? Inua mkono wako. Sasa, kile tutakachofanya: “Ishara hizi zitafuatana na hao, aminini,” kama tu vile alivyoahidi jambo *hili* lingetimia, aliahidi kwamba waaminio wanapaswa kuwekeana mikono, na maombi ya imani yanapaswa kuwaokoa

wagonjwa. Mnaamini hilo? Basi wekeaneni mikono, wekeaneni tu mikono. Haya basi. Sasa, usijiombee mwenyewe, wewe mwombee mtu uliyemwekea mikono, nitawaombee ninyi nyote.

²⁷² Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe kusanyiko hili wakati ubatizo wa Roho Mtakatifu ukiwa juu ya watu hawa. Utusikie, Ee Bwana, utusikie, tunaomba. Tunalaani magonjwa yote. Waaminio hawa wamewekeana mikono. Tunajua ya kwamba Wewe upo hapa, tunajua ya kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, tunajua ya kwamba huwezi kushindwa, tunajua Wewe ulimshinda ibilisi, ukashinda nguvu zake, ukashinda kila enzi na mamlaka. Ulimfunga kila roho mchafu, ukamtoa kila pepo ulipokuwa hapa duniani. Ninakuomba Wewe, Bwana, ya kwamba utayasikia maombi yetu.

²⁷³ Sasa, huku wamewekeana mikono: “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

²⁷⁴ Shetani, ninakuamuru kwa Yesu Kristo, toka ndani ya kila mtu humu ndani walioweka mikono yao, ama, aliyewekewa mikono na mwingine! Ninakuamuru kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, toka kwenye jengo hili, na utoke ndani ya watu, ili wote wapate kwenda nyumbani usiku wa leo na wawe huru, kwa sababu ya Uwepo wa Bwana Yesu Kristo! 

60-0708 Bwana, Sisi Tunataka Kumwona Yesu
Shule Ya Sekondari Ya Juu Ya Klamath Union
Klamath Falls, Oregon Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org